# Nipashe

Jumatano Desemba 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581523

MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com




**OSIMHEN NA DADA YAKE WANASOKA BORA AFRIKA**

UKURASA 21



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji

## SERIKALI YAKIRI

# Vipuri feki vimetapakaa

• **Vifaa** vya umeme navyo majanga... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

**Mabomba** 5,000 yatua, ujenzi wa bomba la mafuta sasa kuanza rasmi



UKURASA WA 4

**NMB** yakusanya mtaji bilioni 400/- mkopo kinamama, miradi mazingira



UKURASA WA 19

**WHO** yaisihi Israel kujali binadamu anayeumwa vitani Gaza





Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, akisonga ugali kwa ajili ya mafundi wanaojenga kituo kipya cha polisi kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu, kinachojengwa kwa nguvu za wananchi, wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 9

**HOFU BARAFU KUTOWEKA MLIMA KILIMANJARO 2050**

SERIKALI imeeleza hofu yake kuhusu kutoweka kwa barafu ya Mlima Kilimanjaro ifikapo mwaka 2050...



## Sensa 2022 ilivyoepusha udanganyifu fidia maafa ya Katesh




UKURASA 4

# Wadau: Taarifa sahihi zitamaliza uzushi afya za viongozi nchini

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YATANGAZA VITA KALI YA POINTI 18 UK.24

**KATUNI** UK.6




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Serengeti Breweries Ltd (SBL), Obinna Anyalebechi (kushoto), akibadilishana mkataba na Mkurugenzi wa UN Global Compact Network Tanzania, Marsha Macatta-Yambi jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutia saini mkataba wa makubaliano ya kukuza uendelevu wa biashara na kuchangia kikamilifu katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yakiri vipuri feki vimetapakaa

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka wananchi kuwa makini na kuzagaa kwa vipuri feki vya magari, pikipiki na vifaa vya umeme kwenye masoko mbalimbali nchini.

Ni angalizo lililotolewa jana na Mkurugenzi wa Kudhibiti Bidhaa wa Tume ya Ushindani (FCC), Khadija Ngasongwa, alipowasilisha mada kwenye mkutano Mkuu wa Shirikisho la Wenye Viwanda nchini (CTI).

Alisema serikali imekuwa inadhibiti kwa kiwango kikubwa uingizwaji bidhaa hizo ingawa wanaoingiza wamekuwa wanabadilisha mbinu mara kwa mara ili kukwepa mkono wa serikali.

"Bidhaa feki zimeongezeka kwenye vipuri vya pikipiki, magari na vifaa vya umeme. Hivi vimejaa sana sokoni kwa sababu mahitaji ya vipuri hivi yamekuwa makubwa sana," alihadharisha.

Alisema ni wajibu wa kila mmoja wakiwamo wafanyabiashara na wenye viwanda na taasisi za serikali kusaidia kuibua wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa bandia na zisizo na viwango.

Alisema bidhaa hafifu zimekuwa zinasababisha anguko la bidhaa halisi sokoni kutokana na kuuzwa kwa bei ya chini, hali ambayo imekuwa inawavutia wateja wengi.

Alisema wazalishaji bidhaa wanapaswa kuweka alama ili kuwezesha walaji kutambua kwa urahisi kati ya bidhaa halisi na zile hafifu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, aliitaka CTI kushirikiana na taasisi za serikali kuwafichua wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa hizo kwenye masoko ya Tanzania.

Alisema bidhaa bandia zimekuwa zinasababisha ushindani usio halali kwenye soko kwa kuwa bidhaa hizo zimekuwa zinauzwa kwa bei rahisi.

"Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) yanaweza kusaidia vita dhidi ya bidhaa bandia kuwa rahisi, hivyo wenye viwanda na wafanyabiashara wajikite kwenye matumizi hayo," alishauri.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, alisema ni vigumu kwa sekta ya viwanda nchini kuwa na ushindani wenye haki wa bidhaa kama kutakuwa na bidhaa bandia zinazoingia kutoka nje ya nchi.

Alisema uchumi hauwezi kukua na kufikia Dira ya Taifa la Maendeleo kama viwanda havitafanya vizuri na kuongeza kuwa kuna haja serikali kushughulikia vikwazo vyote vinavyowakabili wafanyabiashara na wenye viwanda ikiwamo kudhibiti bidhaa feki.

"Tunamshukuru Rais kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara tangu aingie madarakani, tunajua bado kuna mengi ya kufanya lakini uelekeo umekuwa mzuri na sisi tumeona tuseme asante kwa sababu tunajua kuna mengi mazuri yatafanyika," alisema.

Vilevile, aliiomba serikali ipunguze gharama za stempu za kielektroniki kwa kuwa zimekuwa zinaongeza gharama kwa wenye viwanda na wafanyabiashara na kusababisha bei kuwa kubwa na kuwa mzigo kwa walaji.

Mkazi wa Magomeni, Ibrahim Juma, alisema serikali haiwezi kukwepa lawama kwa kuzagaa kwa bidhaa feki kwa kuwa nyingi zinapita kwenye mipaka ambayo kuna taasisi zake za udhibiti.

"Kwenye mipaka yote mamlaka zipo. Inaonekana kuna watumishi wachache wa taasisi za serikali wasio waaminifu ambao wanahusika kwa kiwango kikubwa kushirikiana na hawa watu kuzipitisha," alisema.

Linda John ni mfanyabiashara wa vipuri vya magari na pikipiki eneo la Mwenge, wilayani Kinondoni, alisema tabia ya kupenda vitu vya bei rahisi ndiyo inachochea wafanyabiashara wasiowaaminifu kuingiza bidhaa bandia nchini.

"Wale wafanyabiashara wa bidhaa feki wana fedha nyingi, wanaweza kuhonga idadi kubwa ya watu. Ndiyo maana bidhaa hizi haziishi sokoni na biashara hii haiwezi kuisha kwa sababu ina fedha nyingi sana," alidai.

Mfanyabiashara mwingine wa bidhaa hizo katiak eneo la Mwenge, Isaya Musa, alisema bidhaa hafifu ni chaguo la mteja kwa kuwa wengi wamekuwa wanapendelea vitu vya bei nafuu.

"Bidhaa nyingi halisi zinakuwa na bidhaa hafifu pembeni. Hivyo, mteja anapokuja anaambiwa kabisa kwa mfano ukitaka kipuri hiki hafifu ni Sh. 30,000, chenyewe ambacho utadumu nacho ni Sh. 90,000. Wengi wananunua cha Sh. 30,000," alisema.

# Wadau wataka taarifa za viongozi ili kuepusha uzushi

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa mitandao ya kijamii wameishauri serikali kutoa taarifa za viongozi wanapokwenda nje ya nchi au kutokuonekana hadharani kwa muda mrefu ili kuepuka taarifa za uzushi juu yao.

Wamesema wananchi wana haki ya kuhoji waliko viongozi wao na serikali ina wajibu wa kitoa taarifa na kazi wanazofanya.

Ushauri huo ulitolewa jana ikiwa ni takribani mwezi mmoja tangu kuenea kwa mijadala katika mitandao ya kijamii kuhusu alikokuwa Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango. Kutokujulikana alikokuwa kiongozi huyo wa ngazi za juu serikalini, baadhi ya watu walianza kuhoji huku wengine wakizusha kuwa amefariki dunia.

Jumapili iliyopita, baada ya ukimya wa muda mrefu, alivunja ukimya alipohudhuria ibada katika Kanisa Katoliki Parokia Mwenyeheri Maria Theresa Lendochowska, Kiwanja cha Ndege, Dodoma.

Akizungumza baada ya misa hiyo kwisha, Dk. Mpango alisema alikuwa nje ya nchi akitekeleza kazi maalum na kukemea tabia ya watu kutumia mitandao ya kijamii vibaya kwa kumzushia kifo jambo lililozua taharuki.

Kutokana na hali hiyo, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema serikali itawachukulia hatua kwa mujibu wa sheria waliozusha taarifa hizo za uongo ili kudhibiti matumizi mabaya ya mitandao.

Mhariri wa Kituo cha Mtandaoni cha The Chanzo, Khalifa Said, alisema taarifa za uzushi juu ya kiongozi huyo ni matokeo ya serikali kutotimiza wajibu wake wa kutoa taarifa za safari za viongozi wa serikali.

"Makamu wa Rais ni mtu mkubwa sana hapa nchini. Asipoonekana hata wiki moja lile doa lazima lionekane na wananchi lazima waishinikize serikali kusema aliko. Sasa wanasema kwa namna gani hapo ndipo tatizo linapokuja. Kuondoa haya yote serikali inapaswa kutoa taarifa kwa wananchi mapema," alisema Khalifa.

Alisema kitendo cha serikali kuwachukulia hatua waliosambaza taarifa za uzushi juu ya kifo cha kiongozi huyo ni kuwatisha na kuwanyima uhuru wa kuzungumza badala yake serikali ijifunze kutokana na tukio hilo na kurekebisha walipokosea ili lisitokee tena.

Mkurugenzi wa JamiiForums, Maxence Melo, alisema alitarajia kuona serikali inawashukuru Watanzania kwa kuwajali na kuwapenda viongozi wao pamoja na kuwaelimisha matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii badala ya kuwapa vitisho kuwa watawafikisha kwenye mikono ya sheria.

Alisema mpaka wananchi kuchukua uamuzi kuingia mitandaoni na kuhoji aliko kiongozi huyo kuna jambo ambalo wameliona haliko sawa, hivyo kuishinikiza serikali kutoa kauli kuhusiana nalo.

Melo alisema Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015 kifungu cha 16 inamweka hatiani mtu aliayendika maneno ya uongo akiwa anajua anachokifanya si sahihi, tofauti na walichokifanya Watanzania.

"Sidhani kama ni uungwana Watanzania waliotaka kujua viongozi wao wapo wapi waanze kutishwa kwa kuwaambiwa kwamba watakamatwa, watashughulikiwa wakati mpaka sasa hakuna anayejua Makamu wa Rais alikuwa wapi ilhali kiongozi huyo analipwa kupitia kodi ya wananchi," alisema.

Alisema tukio hilo liwe funzo kwa serikali na ifahamu kuwa wananchi wanawapenda viongozi wao na hawapendi kusikia wamepatwa na mambo mabaya, lakini kukaa kimya wakati kiongozi wa nchi hayupo nchini ni kosa.

"Tupo kwenye mwezi wa haki za binadamu halafu tunaanza kuwatisha binadamu hao hao tunaowaongoza tukidhani tunawatawala tunakosea. Katika mwezi huu tunatarajia serikali iwe mstari wa mbele kulinda haki za binadamu ikiwamo ya kufahamu waliko viongozi wao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Zaina Foundation, shirika lisilo la kiserikali linalotetea haki za kidijitali nchini, Zaituni Njovu, alisema jambo jema kutumia mitandao ya kijamii kutoa taarifa inavyoweza kuleta taharuki kwa jamii kama vile kifo hasa kwa kiongozi mkubwa kama Makamu wa Rais.

Alisema hata kama taarifa hizo zingekuwa za kweli, kuna utaratibu maalum wa kutoa kulingana na cheo cha mtu husika na si kila mmoja kuingia kwenye mitandao na kueneza taarifa aliyoisikia bila kuwa na uthibitisho.

Njovu alisema vitendo hivyo vinaweza kusababisha madhara makubwa kwa ndugu, jamaa na marafiki wa mhusika ikiwamo kupata magonjwa ya moyo, msongo wa mawazo na kukosa raha wakiamini kuwa ni kweli ndugu yao amepatwa na tatizo lililosemwa.

Njovu aliunga mkono kauli ya Waziri Nape Nnauye wa kuagizwa waliosambaza taarifa hizo kupitia kurasa zao za mitandao wakamatwe na sheria ifuate mkondo wake ili kukomesha tabia hiyo.

Alisema kwa sasa kumeibuka tabia ya watumiaji wa mitandao hiyo kusambaza taarifa zenye kuleta taharuki wakiwa na lengo la kujipatia wafuasi wengi katika kurasa zao jambo ambalo si sahihi.

Njovu aliishauri jamii iitumie mitandao katika masuala yatakayowakuza kiuchumi, elimu na kujiletea maendeleo badala ya kusambaza taarifa ambazo baadaye zitawaletea shida na kuishia kwenye mikono ya sheria.




Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu na masuala ya ubia na ushirika Afrika, Simon Shayo akizungumza katika hafla ya kukabidhi tuzo kwa mwajiri bora wa mwaka 2023, zilizoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yatoa msaada waathirika wa mafuriko ya tope Hanang'

**Na Mwandishi Wetu,**
HANANG'

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imekabidhi msaada wa fedha taslimu Sh. milioni 10, chakula, nguo na mablanketi kwa waathirika wa mafuriko wilayani Hanang, mkoani Manyara.

Msaada huo wenye jumla ya thamani ya Sh. milioni 20, pia unajumuisha mchele, maharage, unga na mafuta ya kupikia.

Msaada huo ulikabidhiwa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano ya Umma wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi.

Akizungumza baada ya kukabidhi msaada huo, Semunyu aliyekuwa ameambatana na baadhi ya maofisa wa benki hiyo waliowakilisha wafanyakazi wengine wa benki hiyo, alisema NBC inatoa salamu za pole kwa waathirika wa tukio hilo, serikali na Watanzania kwa ujumla.

Alisema wamepokea kwa huzuni taarifa za athari zilizotokana tukio hilo ikiwamo vifo vya watu na mifugo na upotevu wa mali.

Alisema benki hiyo inaungana na Watanzania kwa ujumla katika kuwafariji waathirika wa tukio hilo kwa hali na mali na zaidi kuwaombea kwa Mungu wote waliojeruhiwa na waliopoteza maisha katika janga hilo. "Tumeamua kutumia kiasi tulichonacho kama taasisi na pia kama wafanyakazi mmoja mmoja kuwasaidia ndugu zetu wanaopitia wakati mgumu kwa sasa kutokana na janga hili baya.

"Pamoja na fedha, pia tumewaletea vyakula mbalimbali ikiwamo unga, mchele, maharage na mahitaji muhimu kama vile mablanketi na shuka ili viwasaidie kwa kipindi hiki cha mpito.

"Pia tunashukuru sana serikali yetu na jamii kwa ujumla kwa kusimama imara na kuonesha ushirikiano mkubwa katika kusaidia waathirika na majeruhi wa janga hili.

"Tumefarijika kuona waathirika wanaendekea kupata faraja kupitia misaada mbalimbali inayoendelea kutolewa na wadau mbalimbali pamoja na serikali. Nasi tunaahidi kuendelea kusaidia zaidi kadri iwekezanavyo," alisema Semunyu.

Akipokea msaada huo, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jimmy Yonaz, aliishukuru Benki ya NBC na wafanyakazi wake kwa kuona umuhimu wa kuwafikia waathirika wa mafuriko hayo, hatua inayothibitisha nia ya dhati ya benki hiyo katika kushirikiana na jamii.

# Mabomba 5,000 yatua, ujenzi wa bomba la mafuta kuanza

**Na Christina Mwakangale**

MATUMAINI ya kuanza kwa ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga, Tanzania, yameongezeka baada ya kuwasili kwa awamu ya kwanza ya mabomba 5,000.

Mabomba hayo yatatosha eneo la kilomita 100 kati 1,443 za mradi huo, yataanza kutandazwa ardhini, Februari, mwakani huku mradi wote ukitarajiwa kukamilika mwaka 2025 na mafuta kuanza kusafirishwa rasmi kwa njia hiyo mwaka 2026.

Mratibu wa mradi huo kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Safiel Msovu, akizungumza baada ya ziara iliyofanywa na wabia wa mradi huo katika kitalu cha kuhifadhi miundombinu hiyo, alisema sasa nia ya Waganda na Watanzania, inatimia.

"Mabomba ya kilomita 100 za kwanza yamewasili nchini kwa maana hiyo mradi uko tayari kuanza utekelezaji wake. Nchi zote mbili zinaonyesha kwamba mradi unatekelezeka. Kwa Tanzania kupitia TPDC kama mwanahisa tumekwishawekeza na hadi sasa zaidi ya Sh. bil. 500 zimechangia mradi.

"Kitakachoendelea baada ya mabomba kuwasili, yataanza kusambazwa na ifikapo Februari, mwakani, yataanza kufukiwa ardhini na mwaka 2025 mradi utakuwa umekamilika na mafuta ya kwanza yataanza kupita mapema 2026," alisema Msofu.

Alisema mabomba hayo yatafikishwa katika kituo kikuu cha miundombinu hiyo, kilichoko Nzega mkoani Tabora, kabla ya kuanza hatua ya kuyafukiwa ardhini mwakani.

Meneja Mradi kutoka Kampuni ya East African Logistic Solutions (EALS) inayosambaza miundombinu ya Kampuni ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Stevan Miller, alisema yamewasili mabomba na hivyo matarajio kuyasafirisha yataanza kwa awamu.

Balozi wa Uganda nchini, Kanali Mstaafu Fred Mwegisye, alisema kwa anawashukuru marais wa nchi hizo mbili kwa kuchukua uamuzi wa pamoja na kupitisha bomba hilo nchini.

"Tunamshukuru Mungu kwa maana tunaona namna watu wake wa Tanzania na Uganda, na wadau wote watakavyonufaika na mradi huu kwa nchi nyingine kama Sweden ambayo inaunda magari maalum ya usafirishaji," alisema Balozi Mwegisye.

"Kila mmoja atakayehusika na mradi huu ni kwamba Mungu amefanya hivyo kwa kusudi lake maalum, matarajio yetu, mustakabali wetu na malengo yetu, yatatimia," aliongeza balozi huyo.

Catherine Mbatia, Mkuu wa Mawasiliano, Kampuni ya East African Crude Oil Pipeline Tanzania, alisema mradi huo, una urefu wa jumla ya kilomita 1,443 kati ya hizo kilomita 296 zipo nchini Uganda na kilomita 1,147 zipo Tanzania.

Alisema bomba hilo, litapita katika mikoa nane ya Tanzania Bara ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga na litapita katika wilaya 24, kata 134 na vijiji zaidi ya 180.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**Ofisi ya Rais**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA VIFAA CHAKAVU

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) itauza kwa njia ya mnada wa hadhara Magari chakavu katika Mkoa wa Dar es Salaam na Mbeya katika vituo na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

| Na | AINA YA GARI ZITAKAZOUZWA | IDADI | KITUO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Landrover Defender 110 | 17 | TASAF OFFICE DSM | 21/12/2023 |
| | Land rover 90 | 13 | | |
| | Suzuki Garnd | 2 | | |
| | Nissan Patrol | 1 | | |
| 2 | Landrover Defender 110 | 18 | VETA KEKO DSM | 22/12/2023 |
| | Landrover 90 | 17 | | |
| | Suzuki Grand Vitara | 4 | | |
| 3 | Landrover Defender 110 | 1 | ILEJE MBEYA- OFISI YA HALMASHAURI | 23/12/2023 |
| | **JUMLA** | **73** | | |

**MASHARTI YA MNADA**

i. Gari itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo
ii. Mnunuzi atalazimika kulipa papo hapo amana (Deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya gari atakayonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa gari husika na amana iliyolipwa haitarudishwa.
iii. Mtu yoyote atakaetamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
iv. Mnunuzi atatakiwa kuondoa gari atakayonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe ya kukamilisha malipo.
v. Ruhusa ya kuangalia magari yanayokusudiwa kuuzwa itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada husika
vi. Mnada utaanza saa nne kamili (04:00) asubuhi katika kila kituo.

**Kaimu Mkurugenzi Mtendaji**
**Mfuko wa Maendeleo ya Jamii – TASAF**
**Barabara ya Jakaya Mrisho Kikwete**
**S. L. P 2719 Dodoma,Tanzania**
**Simu: 255 026 2963866**
**Nukushi: 255 026 2963871**
**Barua pepe: info@tasaf.go.tz**
**Tofuti: www.tasaf.go.tz**

177437




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo (katikati), akigonga kengele kuashiria kuorodhesha rasmi hati fungani ya NMB Jamii katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) jana. Wengine ni Balozi wa Uingereza nchini, David Concar (kushoto), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Nichodemus Mkama (wa pili kushoto), Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Mary Mniwasa (wa pili kulia) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yakusanya bilioni 400/- kukopesha miradi mazingira, nishati safi, wanawake

## •Hisa zawekwa sokoni DSE, serikali yapongeza

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeweka rekodi ya makusanyo ya Sh. bilioni 400 za mauzo ya toleo la kwanza la Hati Fungani ya Jamii (NMB Jamii Bond), ambayo ni sehemu ya Programu ya Muda wa Kati. Hati Fungani hiyo sasa imeorodheshwa rasmi katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE).

Hati Fungani ya Jamii ya NMB ilizinduliwa na kuanza kuuzwa Septemba 25 hadi Oktoba 27 mwaka huu, ikilenga kukusanya Sh. bilioni 75 na ongezeko la Sh. bilioni 25 na hivyo kuwa na idhinisho la jumla la Sh. bilioni 100, huku mauzo kwa Dola za Marekani yaliyoidhinishwa yakiwa ya Dola milioni 10 na ongezeko la Dola milioni tano.

Wakati wa kutangaza matokeo ya Hati Fungani hiyo na kuiorodhesha DSE, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema ilikusudia kukusanya fedha kwa ajili ya kutoa mikopo inayolenga matokeo chanya na endelevu katika jamii ya Watanzania, ikiwamo miradi ya nishati mbadala.

"Hili ni toleo la kwanza la mauzo ya NMB Jamii Bond yaliyokuwa yamegawanyika katika mafungu mawili; fungu la kwanza likihusisha Shilingi za Kitanzania na fungu la pili la Dola za Kimarekani, ambako kote tumevuka lengo la makusanyo.

"Kwa upande wa Shilingi, tumepata bilioni 212.9 kutoka Sh. bilioni 100 za lengo na upande wa Dola tukikusanya milioni 73 badala ya Dola milioni 15.

"Kwa mantiki hiyo, thamani ya jumla ya fedha zilizopatikana kutokana na NMB Jamii Bond ni Sh. bilioni 400, ambazo ni mara tatu zaidi ya lengo tulilokuwa nalo, ili kuwezesha pamoja na kutoa mikopo inayolenga matokeo chanya na endelevu kwa jamii. Fedha hizi zitatumika katika miradi ya kuzuia na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.

"Miradi mingine itakayonufaika ni ile ya usimamizi wa maji safi na maji taka, miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuwawezesha wanawake na usawa wa kijinsia, nyumba nafuu, usalama wa chakula, huduma za afya, elimu na vijana," alibainisha Zaipuna huku akiwahakikishia wateja 5,600 walionunua hati fungani hizo kuwa fedha zao ziko kwenye mikono salama.

Mbele ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, Zaipuna alisema wanajivunia mtandao mpana wa matawi ya benki yake kwa kufanikisha mauzo ya asilimia 99.9, huku asilimia 0.1 ikiuzwa kupitia madalali wa Mamlaka ya Masoko na Mitaji na Dhamana (CMSA).

"Hatimaye leo (jana) tunaiorodhesha rasmi hati fungani hii hapa DSE, ili kutoa fursa kwa walionunua kuziuza kwa waliozikosa kipindi cha mwezi mmoja, ambako kwa wawekezaji walionunua kwa Shilingi watapata riba ya asilimia 9.5 watayolipwa kila baada ya miezi mitatu na wawekezaji wa Dola watalipwa kila baada ya miezi sita, yaani mara mbili kwa mwaka," alisema Zaipuna.

Katika hafla hiyo, Prof. Mkumbo alipongeza NMB kwa kuweka rekodi ya Sh. bilioni 400 za mauzo ya hati fungani hiyo.

Alisema utaratibu huo si tu unaunga mkono juhudi za serikali kuongeza idadi ya Watanzania walio kwenye mifumo rasmi ya kibenki, bali pia kwa kuchagua kukopa kwa wananchi badala ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ama benki za kimataifa.

"Hati fungani ni fursa muhimu kwa jamii kunufaika kwa njia mbili za kuweka akiba, lakini pia kufanya uwekezaji wenye faida kubwa. Hati fungani ni mkopo ambao taasisi ya fedha inakopa kwa wananchi. NMB ingeweza kwenda kukopa BoT au benki za nje, lakini ikachagua kukopa kwa wananchi kupitia mdhamana wao ambaye ni CMSA na inarejesha kwa riba kubwa ya asilimia 9.5.

"Pongezi zangu kwa NMB pia kutokana na unyeti na umuhimu maeneo wanakozielekeza fedha hizi, kwa sababu mnakwenda kuisaidia pakubwa sana serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Pia ninakiri kwamba hati fungani hii imeniheshimisha mno mimi kwa Rais, kwani imeingiza Dola za Marekani milioni 73 katika kipindi hiki cha uhaba wa Dola nchini.

"Rekodi hii ya mauzo inaweza kuwa ya kushangaza kwa taasisi zingine, lakini kwa NMB hili si la kushangaza kutokana na ufanisi wake, ikitajwa mara 10 na majarida ya Euromey, Global Magazine, African Bankers na mengine kuwa ni Benki Bora na Salama Zaidi Tanzania, huku Ofisa Mtendaji Mkuu wake akitwaa tuzo kadhaa za CEO (Ofisa Mtendaji Mkuu) Bora wa Mwaka wa Afrika," alisisitiza Prof. Kitila.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, Nicodemus Mkama, alisema NMB imefanya mapinduzi makubwa katika sekta ya masoko na mitaji ya dhamana kwa kuingiza kiasi kikubwa cha fedha za mauzo ya hati fungani yake, ambayo inaipa heshima mamlaka yake, benki hiyo na taifa kwa ujumla nje ya mipaka ya Tanzania.

"Hati fungani hii inaweka rekodi ya kuwa ya kwanza kwa jamii kuwahi kuelekezwa katika miradi endelevu ya kijamii na ni hatua muhimu mno katika maendeleo na ustawi wa sekta ya fedha Tanzania kuunga mkono juhudi za serikali za kujenga mazingira wezeshi na shirikishi ya kisera, kisheria na kiutendaji na kuchochea ukuaji wa sekta hiyo na uchumi kwa jumla.

"Mauzo ya hati fungani hii yamekuwa na mwitikio mkubwa, unaothibitisha kukua kwa kiwango cha uelewa wa wananchi kuhusu uwekezaji katika masoko ya fedha nchini, kama tuilivyoona kwamba asilimia 98.7 ni wawekezaji mmoja mmoja na asilimia 1.3 tu ya wawekezaji 5,600 ndio taasisi. Takwimu hizi ni muhimu kwa ongezeko la ukwasi katika soko," alisema Mkama.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Mary Mniwasa, aliipongeza NMB kupeleka sokoni Jamii Bondi, ambayo inakwenda kuliongezea thamani Soko la Hisa la Dar es Salaam, ambalo limelazimika kurekebisha mifumo yake ili kuruhusu mauzo ya hisa kwa Dola za Kimarekani, ambayo awali halikuwa nayo.

"Mpaka sasa DSE imeorodhesha hati fungati 27. Hii ya NMB ni ya 28 kutoka kwa kampuni 15, nyingi zimeiva na kwa sasa ziko saba ya NMB ya nane, hizo zingine zitaiva kuanzia Juni (mwakani).

"Hati fungani hii ya NMB inakwenda kuongeza thamani ya hati fungani sokoni za Sh. bilioni 326 Oktoba mwaka huu hadi Sh. bilioni 538, ongezeko la asilimia 25 la fedha za kigeni.

"Lakini kwa mara ya kwanza katika historia yetu, NMB wametuletea hisa za fedha za kigeni, awali mifumo yetu iliitengenezwa kuuza hisa kwa Shilingi za Kitanzania tu.

"Kwa hiyo, NMB Jamii Bond ikatulazimisha kuwaingiza wataalamu wetu kazini kurekebisha mifumo na sasa rasmi tunaanza na Dola milioni 73 za NMB," alibainisha.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali, wakiwamo Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, Mwakilishi wa Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Mihaela Marcu, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Uhifadhi wa Dhamana (CSDR), Benitho Kyando na Mkurugenzi wa Taasisi ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha Afrika (FSD Africa), Evans Osano.

## Sensa ilivyoepusha udanganyifu fidia maafa ya Katesh

**Na Maulid Mmbaga**

KAMISAA wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, Anne Makinda amesema takwimu zinazotokana na sensa hiyo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kuepusha udanganyifu wakati wa kuratibu misaada kwa wananchi waliopatwa na majanga ya mafuriko wilayani Hanang, mkoani Manyara.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa semina iliyoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa lengo la kuwaongeza uelewa viongozi wa dini juu ya namna ya kutumia matokeo ya sensa.

Spika huyo wa zamani wa Bunge alisema takwimu hizo pia zimesaidia rasilimali za nchi kwenda pale zinakohitajika na kutumika kwa usahihi.

Alisema katika sensa hiyo kulipigwa picha za satelaiti nchi nzima na kuonesha kila kitu kilipo kwa uhalisia wake ikiwamo makazi, watu, mali na hali zao za kimaisha. Kumewasaidia kutoa msaada kwa kijamii wilayani Hanang' kwa usahihi.

"Haya maafa yaliyotokea Hanang', sensa imesaidia kwa sababu unajua kunapotokea matatizo watu wanafikiria ndio njia ya kujinufaisha wenyewe, wanakuambia tuko idadi hii, kumbe sensa inasema wako idadi hii na nyumba zinaonekana.

"Mtu anasema nyumba yangu ilikuwa imejengwa kwa matofali na kuezekwa kwa bati, wakati kumbe aliezeka na majani na alijenga kwa udongo ikaondoka.

"Mpaka kesho sensa itasaidia, tumefanya mafundisho sehemu nyingi na kuelekeza wenzetu matumizi ya matokeo na tunakuja na ramani ya kila sehemu, na inawafanya wananchi wawajibike kimaendeleo," alisema.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alibainisha kuwa kutokana na majanga yaliyotokea Hanang', takwimu za sensa zilisaidia vyombo vya usalama kufanya kazi yake kwa uhakika zaidi bila kubahatisha.

Alisema takwimu za sensa ziliwasaidia kujua kila eneo kuna nyumba gani, kaya ngapi, wahusika wa kaya hizo ni kina nani, walioipatikana hai ni nani na waliokuwa hawaonekani ni kina nani.

"Lakini hata huduma zingine zinazoendelea sasa za kuhakikisha wale waliopata athari wanapatiwa huduma zingine za ziada, ikiwamo makazi mengine ya kudumu, zimechangiwa kwa kiasi kikubwa na utaratibu wa sensa iliyofanyika katika kipindi hiki.

"Kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ninaipongeza sana NBS pamoja na makamisaa kwa kazi kubwa na nzuri mliyofanya ya kutusaidia kupata takwimu za sensa ambazo zinakwenda kusaidia pia katika kuimarisha usalama wa nchi yetu," alisema.

Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Omari, alisema sensa hiyo itaonesha namna wanavyokwenda kufanikisha mipango waliyojipangia kuifanya kwa kipindi chote wanachotoa huduma za kiroho katika jamii.

Kasisi wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dar es Salaam, Fadha Julius Kiondo, alisema takwimu za sensa hiyo zitawasaidia pia katika kupeleka huduma mbalimbali za kiroho katika jamii inayowazunguka.

## HABARI KITAIFA

# Wataka uzalendo utawala bora dira 2050

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wameshauri Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kutilia mkazo masuala mbalimbali yakiwamo uzalendo, kujenga nguvu kazi yenye ujuzi, utawala bora, sera ya kulinda sekta binafsi, kinga ya kiuchumi ya nchi, mapinduzi ya kilimo na viwanda.

Akizungumza kuhusu mchango wa sekta binafsi kwenye mjadala wa kitaifa wa miaka 62 ya Uhuru na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 uliofanyika kwa njia ya mtandao, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Raphael Maganga, alisema sekta binafsi bado ni changa na imepiga hatua kubwa ndani ya miaka 62 ya Uhuru.



Alisema uwekezaji katika miundombinu ikiwamo usafiri wa anga na kujengwa kwa reli ya kisasa (SGR) umechangia kukua kwa sekta hiyo na wafanyabiashara wameendelea kukua.

"Ushirikishwaji wetu katika dira ya 2025 umekuwa mzuri. Sekta binafsi imetambulika kama mwajiri mkubwa kwa Watanzania na katika dira ya 2050 tuwe na sera zinazolinda sekta binafsi kwa kuwa bado changa ikilinganisha na sekta nyingine zinazoshindana nazo kimataifa," alisema.

Alisema wafanyabiashara wawezeshwe kuwa na ushindani wa kufungua ushindani wa kimataifa, kuwa na sera ambazo zitakinga uchumi wa Tanzania pale inapotokea majanga.

### UTAWALA BORA

Naye Mwenyekiti wa Chama cha NCCR - Mageuzi, Joseph Selasini, alishauri katika dira ijayo utawala bora utiliwe mkazo kutokana na kukithiri kwa vitendo vya rushwa.

"Lazima vyama vihakikishe vinakuwa na utaratibu wa kuimarisha utawala bora ndani ya vyama na kuchagua watu ambao wana sifa na uadilifu na kusimamia rasilimali za nchi vizuri," alisema.

Selasini alisema wanufaika wakubwa wako sekta ya kilimo na kwamba kuna haja ya kukifanya kilimo kuajiri vijana wengi na kusisitiza dira ielekee kwenye mapinduzi ya kilimo na viwanda.

"Tutengeneze mipango ambayo tutatumia bahari yetu vizuri. Sisi vyama vya siasa tuko tayari kuhamasisha wanachama wetu kushiriki kwenye mchakato huu waseme nini wanahitaji na kwa ushirikiano huu itatengenezwa dira shirikishi," alisema.

Mmoja wa wachangiaji kwenye mjadala, Salum Bakari kutoka Zanzibar, alipendekeza dira ijikite katika nguvu kazi na iwe na ubunifu uliobora ili kuzalisha ajira nyingi.

"Pia tujenge uzalendo bila uzalendo hatuwezi kufikia maendeleo yetu maana hata mataifa yaliyoendelea wananchi wao wamejengwa kwenye misingi ya uzalendo. Pia kuwe na uendelevu wa kaulimbiu kama Tanzania tunategemea miaka 50 mbele tufike wapi kama ni eneo la viwanda au kilimo," alisema.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya wana Diaspora, Norman Jasson, alisema katika utawala bora inapaswa viongozi waliopewa dhamana watimize wajibu wao kuhudumia wananchi bila upendeleo.

"Tunaomba Diaspora washiriki katika kuandika dira hii na washirikishwe kwenye mpango mzima wa mchakato ili tujisikie tupo pamoja, kushirikishwa kwenye sekta ya kiuchumi kupitia sekta binafsi," alisema.

Hata hivyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, aliwahakikishia Watanzania watakuwa na ushiriki mpana kwenye utoaji wa maoni namna Tanzania wanayoitaka miaka ijayo.

Akitoa mada ya ushiriki wa makundi maalum kwenye dira, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alisema hakuna kundi litakaloachwa nyuma kwenye ukusanyaji wa maoni.

"Watanzania tuungane kwenye kupinga rushwa na tutakapokuja kukusanya maoni mtupe maoni tutayafanyia kazi kwa ajili ya mustakabali wa taifa letu," alisema.

### MIKAKATI ZANZIBAR

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, akizungumzia mafanikio ya utekelezaji wa dira ya Zanzibar, alisema iko dira ya maendeleo ya mwaka 2050 na iko katika hatua ya kwanza kwenye utekelezaji.

Alisema uchumi wa Zanzibar kwa sasa unakua baada ya tatizo la ugonjwa wa Uviko -19 na wamejipanga kuongeza uzalishaji wa bidhaa ili kuondokana na kuagiza nje ya Zanzibar.

"Tumedhamiria kutengeneza viwanda vidogo vidogo na tunataka katika kutekeleza sera yetu ya uchumi wa bluu tunataka kuongeza uzalishaji wa karafuu, tuongeze thamani kwa zao la mwani, bidhaa za viungo pia," alisema.

### MAISHA BORA

Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango ya Taifa, Lawrence Mafuru, alisema taifa linapanga namna ya kutumia rasilimali na mambo yanayopaswa kushughulikiwa.

Alisema Dira ya mwaka 2025 ilitaka kuwa na maisha bora kwa watanzania na litaendelea kubaki kuwa la muhimu kwa serikali kwa miaka mingi ijayo.

"Pia kuwa na uchumi wa viwanda shindani, mataifa yanashindana kwa mitaji ya uwekezaji, kuvutia wawekezaji na kuuza bidhaa nje na hili lilikuwa miongoni mwa malengo matano ya Dira ya 2025," alisema.

Alisema kumekuwa na mafanikio katika dira hiyo inayomaliza muda wake ikiwamo umaskini wa kupindukia umeshuka kutoka asilimia 19 Mwaka 2000 hadi asilimia tisa kwasasa.

"Tunawatanzania ambao wameelimika wanaendesha maisha yao na kushindana kwenye maeneo mbalimbali ya dunia, ukuaji wetu wa uchumi umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia sita kwa miaka 20 iliyopita ikilinganishwa na mataifa mengine yaliyoendelea,"alisema.

Kadhalika, alisema katika ukusanyaji wa maoni ya Dira ya 2050 zipo njia mbalimbali za kuhakikisha makundi yote ya watanzania yanafikiwa na kuamua mustakabali wa nchi yao wanataka Tanzania ya aina gani.

Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dk.Tausi Kida, alisema mipango ya Halmashauri, Mikoa na Taasisi inatakiwa ilingane na mpango wa muda mrefu na wakati ambao unatekeleza dira.

"Tuwe na malengo yanayotekelezeka kwa kuangalia uhalisia wa nchi yetu, jambo jingine tunapopita kwenye dunia ya utandawazi tuangalie mila na desturi zetu kwenye dira hii mpya lazima haya yaangaliwe," alisema.


## UNAUDITED RESULTS FOR THE QUARTER ENDED 30 SEPTEMBER 2023

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

**Introduction**

**Dear Shareholders,**

We hereby present the unaudited annual results of Tanga Cement Public Limited Company ("Tanga Cement" or the "Company") and its subsidiary (together, the "Group") for the quarter ended 30th September 2023.

Amidst the escalating competitive dynamics prevalent in the industry, the inadequate electricity provisioning, and the scarcity of major foreign currencies like US Dollars and Euros in the money market, the operational performance of the group has exhibited a favourable improvement compared to the corresponding period in the prior year's third quarter. The group navigated through marketing and operational impediments stemming from persistent power disruptions and an atypical season of heavy rainfall, both of which carried the potential to adversely influence the group's financial metrics during the quarter. The Financial and Operational Overview below provides a comprehensive overview of the group's performance.

We affirm our commitment to all stakeholders through our high-quality cement and clinker, and our contribution towards the sustainable growth and development of Tanzania, a demonstration of our brand – "Strength Within".

The company has deployed the highest standards of health and safety protocols across all its operations and continues to enforce safety at the workplace to protect our employees and contractors.

**Macro-economic Overview**

The Group's growth hinges on Tanzanian construction industry demand for cement, supported by improved economic performance with a 5.7% GDP growth in 2023. Despite a slight decline in the inflation rate to 3.3% in Q3 2023, robust infrastructure investment and a growing consumer base are primary performance drivers. The Group is optimistic about the Government's Development Vision 2025 program's positive impact on infrastructure development, expecting continued momentum in 2023.

**Financial and Operational Overview**

In the third quarter of 2023, the company demonstrated robust financial performance with a notable 12% increase in sales revenue compared to the same period in 2022, reaching TZS 63.5 billion. This growth was accompanied by a substantial 38% surge in gross profit over the same quarter in the prior year, reaching TZS 15.6 billion, attributed to improved gross margins resulting from the company's commitment to efficiency through marginal price adjustments and effective cost containment strategies. Despite challenges such as power outages impacting production, EBITDA also showed a remarkable 57% growth, reaching TZS 9.2 billion. The intentional implementation of cost containment strategies by the management played a pivotal role in achieving these positive results.

However, the Group reported an overall loss before tax of TZS 16.8 billion in Q3, 2023, compared to a loss of TZS 1.7 billion in the same period in 2022. This increase in pre-tax loss is primarily attributed to higher interest expenses on term loans and foreign exchange losses, influenced by the weakening Tanzanian Shilling against the US Dollar. On a positive note, cash generated from trading activities and net cash flows from operations experienced significant increases of 220% and 470%, respectively, showcasing the effectiveness of the company's cashflow management and cost containment strategies in improving the overall financial metrics. Despite these challenges, the Group remains committed to its sales, logistics, and cost optimization initiatives, maintaining a positive outlook for 2023 amidst a competitive landscape and global geopolitical unrest.

**Dividend**

The company did not declare an interim dividend to shareholders in 2023 to remain prudent with available cash resources in order to remain sustainable through the global economic uncertainties and the high fuel prices coupled with pronounced scarcity of major foreign currencies affecting the local economy. The board has decided to continue committing available cash generated to operational commitments. Having regard to the significant increase in Loss of Tax, it remains unlikely that the company will declare a final dividend for the 2023 financial year.

**Proposed acquisition by Scancem International DA**

Shareholders are reminded of the announcement regarding the proposed acquisition by Scancem International DA of 68.33% of the shares in Tanga Cement PLC from Afrisam Mauritius Investment Holdings Limited on 27 October 2021 and the update issued by the Company on 24 April 2023.

On 10 November 2023 an Extraordinary Meeting of Shareholders approved the transaction by a significant majority vote and the parties have concluded the transaction with effect from 27 November 2023.
The resulting acquisition of the controlling shareholding in Tanga Cement PLC by Scancem International DA, a subsidiary of the Heidelberg Materials group will allow Heidelberg Materials to further strengthen its long-standing presence in the cement industry in Tanzania, unlocking value for our present and future shareholders, our employees, customers and other stakeholders.

**Conclusion**

Tanga Cement remains grateful to its staff for their passion and dedication to the company, and to its customers for their belief in the Simba Cement brand, as the company works to achieve its short- and long-term growth strategy.

With Tanzania remaining a significant player in the East African construction market, cement output is anticipated to increase and Tanga Cement is well positioned to take advantage of the growth opportunities in the regional market.

For and on behalf of the Board

**Hakan Gurdal**
Chairman of the Board

| Consolidated and separate statements of profit or loss and other comprehensive income FOR THE PERIOD ENDED 30 SEPT 2023 | Group Sep-23 TZS'000 | Group Sep-22 TZS'000 | Company Sep-23 TZS'000 | Company Sep-22 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 63,545,094 | 56,961,059 | 63,545,094 | 56,961,059 |
| Cost of sales | (47,928,265) | (45,653,790) | (47,928,265) | (45,653,790) |
| **Gross profit** | **15,616,830** | **11,307,268** | **15,616,830** | **11,307,268** |
| Selling expenses | (1,056,838) | (787,510) | (1,056,838) | (787,510) |
| General and Administration expense | (10,011,717) | (9,354,979) | (9,960,209) | (9,355,670) |
| **Operating profit** | **4,548,276** | **1,164,780** | **4,599,783** | **1,164,088** |
| Interest expense | (6,943,833) | (4,816,869) | (6,945,661) | (4,820,540) |
| Finance and Other income | 1,793,680 | 23,008 | 1,754,240 | 25,951 |
| Foreign exchange and fair value (losses)/gains | (16,185,637) | 1,968,943 | (16,185,637) | 1,959,732 |
| **Loss before tax** | **(16,787,514)** | **(1,660,139)** | **(16,777,275)** | **(1,670,770)** |
| Income tax (charge)/credit | (367,536) | 245,932 | (367,536) | 245,932 |
| **Loss for the period** | **(17,155,050)** | **(1,414,207)** | **(17,144,811)** | **(1,424,838)** |
| **Total comprehensive income for the year attributable to:** | | | | |
| Owners of the parent | (17,155,050) | (1,414,207) | (17,144,811) | (1,424,838) |
| Non-controlling interests | - | - | - | - |
| | **(17,155,050)** | **(1,414,207)** | **(17,144,811)** | **(1,424,838)** |
| | **Sep 23 TZS/share** | **Sep 22 TZS/share** | | |
| Basic and Diluted loss per share | **(272)** | **(22)** | | |

| Consolidated and separate statements of financial position AS AT 30 SEPT 2023 | Group Sep-23 TZS'000 | Group Sep-22 TZS'000 | Company Sep-23 TZS'000 | Company Sep-22 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | | |
| **Non-current assets** | | | | |
| Property, plant and equipment | 278,546,758 | 290,915,133 | 277,827,542 | 290,105,944 |
| Right-of-use assets | 4,510,244 | 4,904,924 | 4,477,927 | 4,817,032 |
| Investment property | 497,982 | 543,438 | - | - |
| Investment in subsidiary | - | - | 420,995 | 552,564 |
| Financial asset - Interest rate cap | 6,841,115 | 7,086,737 | 6,841,115 | 7,086,737 |
| Deferred tax asset | (950,784) | - | (950,784) | - |
| | **289,445,315** | **303,450,231** | **288,616,794** | **302,562,277** |
| **Current assets** | | | | |
| Due from employees' share trust | - | - | 773,467 | 773,467 |
| Inventories | 94,927,062 | 73,200,801 | 94,927,062 | 73,200,801 |
| Trade and other receivables | 6,130,679 | 12,467,255 | 6,430,983 | 12,476,140 |
| Current income tax recoverable | 8,729,751 | 732,675 | 8,243,317 | 177,863 |
| Cash and bank balances | 9,395,718 | 8,003,520 | 9,354,786 | 7,729,596 |
| | **119,183,210** | **94,404,250** | **119,729,616** | **94,357,868** |
| Non-current assets held-for-sale | - | 3,870 | - | - |
| **TOTAL ASSETS** | **408,628,525** | **397,858,351** | **408,346,410** | **396,920,145** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | | | |
| **Equity** | | | | |
| Issued capital | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 |
| Translation reserve | - | (67,490) | - | - |
| Treasury shares | (773,466) | (773,466) | - | - |
| Retained earnings | 88,584,823 | 134,465,366 | 86,899,944 | 133,062,927 |
| **Equity attributable to owners of the parent** | **89,084,778** | **134,897,830** | **88,173,365** | **134,336,348** |
| Non-controlling interest | - | - | - | - |
| **Total equity** | **89,084,778** | **134,897,830** | **88,173,365** | **134,336,348** |
| **Non-current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 4,059,448 | 4,193,853 | 3,964,842 | 4,386,852 |
| Provision for site restoration | 30,014 | 29,637 | 30,014 | 29,637 |
| Term borrowings: Non-current portion | 242,399,262 | 203,866,126 | 242,399,262 | 203,866,126 |
| Deferred tax liability | - | (832,413) | - | (832,413) |
| | **246,488,724** | **207,257,202** | **246,394,117** | **207,450,202** |
| **Current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 606,583 | 626,668 | 592,448 | 449,652 |
| Trade and other payables | 46,460,683 | 26,785,398 | 46,838,278 | 26,032,245 |
| Contract liabilities | 7,459,633 | 9,027,263 | 7,820,078 | 9,387,708 |
| Bank overdrafts | 18,528,124 | 19,263,991 | 18,528,124 | 19,263,991 |
| | **73,055,023** | **55,703,319** | **73,778,928** | **55,133,595** |
| **Total liabilities** | **319,543,747** | **262,960,521** | **320,173,045** | **262,583,797** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **408,628,525** | **397,858,351** | **408,346,410** | **396,920,145** |

| Consolidated and separate statements of cash flows FOR THE PERIOD ENDED 30 SEPT 2023 | Group Sep-23 TZS'000 | Group Sep-22 TZS'000 | Company Sep-23 TZS'000 | Company Sep-22 TZS'000 |
|---|---|---|---|---|
| **OPERATING ACTIVITIES** | | | | |
| Cash generated from operating activities | 12,217,220 | 3,822,110 | 12,479,600 | 3,275,288 |
| Interest income received | 2,585,419 | 1,190 | 2,585,419 | 1,190 |
| Income taxes paid | (1,622,605) | (1,511,687) | (1,622,605) | (1,511,687) |
| **Net cash flows from operating activities** | **13,180,034** | **2,311,613** | **13,442,415** | **1,764,790** |
| **INVESTING ACTIVITIES** | | | | |
| Proceeds from sale of property, plant and equipment | - | 35,476 | - | 35,476 |
| Purchase of property, plant and equipment | (5,188,574) | (4,136,339) | (5,188,574) | (4,136,339) |
| **Net cash flows used in investing activities** | **(5,188,574)** | **(4,100,863)** | **(5,188,574)** | **(4,100,863)** |
| **FINANCING ACTIVITIES** | | | | |
| Principal repayments - lease liabilities | (836,373) | (945,921) | (836,373) | (945,921) |
| Lease liability interest paid | - | - | - | - |
| Interest paid - overdrafts | (1,415,259) | (1,221,588) | (1,415,259) | (1,221,588) |
| **Net cash flows used in financing activities** | **(2,251,632)** | **(2,167,509)** | **(2,251,632)** | **(2,167,509)** |
| **Net increase/(decrease) in cash and cash equivalents** | **5,739,828** | **(3,956,758)** | **6,002,209** | **(4,503,581)** |
| Net foreign exchange differences | (344,439) | (592,843) | (589,433) | (254,940) |
| Cash and cash equivalents at 1 January | (14,527,795) | (6,710,870) | (14,586,114) | (6,775,873) |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | **(9,132,406)** | **(11,260,471)** | **(9,173,338)** | **(11,534,394)** |

**Hakan Gurdal**
Chairman
01 DECEMBER 2023

**R Swart**
Managing Director

**Q Ganijee**
Company Secretary

**Tanga Cement Public Limited Company**
P O Box 5053
Tanga
Tanzania
info@simbacement.co.tz

SYSTEM CERTIFICATION ISO 9001 SGS

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# PBPA inavyookoa mabilioni uagizaji mafuta

**WAKALA** wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA), imefanya jitihada kubwa kuhakikisha pesa zilizokuwa zikipotea kutokana na msongamano wa meli zilizokuwa zikisubiri kushusha mafuta bandarini zinaokolewa.

Kwa mujibu wa Mtendaji Mkuu wa PBPA, Wakala huo umeokoa zaidi ya Sh. bilioni 425 kwa kupunguza msongamano wa meli bandarini baada ya kuimarisha Mfumo wa Uingizaji Mafuta kwa Pamoja wa Mafuta nchini (BPS).

Kila mwezi Wakala huo unaokoa Sh. bilioni 4.1 kwa kudhibiti upotevu wa mafuta kwenye meli na mahala ya kuhifadhi nishati hiyo nchini.

Ukusanyaji wa mapato ya kikodi umeongozeka kutokana na kupunguza vitendo vya ukwepaji kodi kwa njia ya udanganyifu.

Mfumo wa ukusanyaji mapato umedhibiti udanganyifu wa gharama za mafuta katika Soko la Dunia na gharama za kuleta mafuta nchini.

Wakala huo umsema Tanzania ina maghala 22 ya kuhifadhi mafuta yenye uwezo wa kupokea kutoka kwenye meli zinazotoka nje na kuingia nchini.

Katika Bandari ya Dar es Salaam kwa upande wa Kurasini kuna maghala 11 yenye uwezo wa kupokea takribani lita milioni 570, Kigamboni manane yenye uwezo wa kupokea lita milioni 522.

Katika Bandari ya Mtwara kuna maghala mawili yenye uwezo wa kupokea takribani lita milioni 35 na Bandari ya Tanga moja lenye uwezo wa kupokea takriban lita milioni 182.

Serikali kwa upande wake inaendelea kuhamasisha wawekezaji kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa kiwango kikubwa cha nishati hiyo nchini.

Wakala huo umehakikisha kuwa nchi haiwezi kupata mtikisiko wa kukosekana mafuta kwa kuwa kwa mujibu wa sheria ni lazima kuwe na hifadhi yanayoweza kutumika kwa siku 15.

Utaratibu wa uagizaji mafuta kwa pamoja hufanyika kwa uwazi kwa waagizaji kukaa pamoja na zabuni kutolewa kwa uwazi.

Wakala huo umefafanua kuwa mikataba ya uagizaji wa mafuta nchini, hutumia tathmini ya bei ya soko inayofanywa Kampuni ya S&P Global yenye ofisini yake nchini Afrika Kusini ambayo hutumiwa na nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika kupata bei ya mafuta katika Soko la Dunia.


Pamoja na mafanikio makubwa ya mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja zipo changamoto zinazosababisha meli za mafuta kuingia nchini kutokana na majanga ya ugonjwa au vita.

Baadhi ya changamoto baada ya mabadiliko ya sera ni kukosekana kwa sheria na kanuni za kusimamia sekta ndogo ya mafuta katika kipindi cha soko huria.

Kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Julai 2022 hadi Desemba 2022, serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iliweka ruzuku ya maputa ili kupunguza bei kwa wananchi na iwe stahimilivu kutokana na kupaa katika soko la dunia baada ya kuzuka kwa vita ya Urusi na Ukraine.

Changamoto nyingine ni kuibuka kwa wimbi la uwekezaji ulio chini ya kiwango katika miundombinu ya mafuta katika mkondo wa chini na uchakachuaji wa mafuta kwa kuchanganya mafuta ya taa na ya dizeli.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Restuta James

# 'No' kupiga kura isiwe 'yes' kwenye ndoa

**MTOTO** ni mtoto bila kujali hali yake ya maisha, hadhi ya familia yake au mazingira aliyopo tena anapaswa kulindwa na sheria ili kuleta usawa kwenye jamii.

Nasema hivyo nikipendekeza marekebisho ya vifungu namba 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971, vinavyoruhusu mtoto kuoa na kuolewa akiwa na umri wa miaka 14 na 15. Binafsi naungana na wanaopendekeza umri wa kuolewa uwe zaidi ya miaka 18.

Kwa nini iwe miaka 18? Ni kwa sababu mtu mwenye umri chini ya miaka hiyo haruhusiwi kuingia mkataba, kupiga kura, kuajiriwa wala kupewa leseni ya udereva, tena hajapewa kibali cha kuwa kiongozi iwe kwenye dini au hata kwenye siasa.

Pia sheria ya elimu inamlinda mtoto aliye shuleni mwenye hadi miaka 18 ambaye pengine anaweza kuwa kidato cha sita, haruhusiwi kuolewa. Lakini ni ajabu mtoto wa miaka 14 anaweza tu kuolewa kwa sababu yuko nje ya shule, jamani tutafakari njia zetu.

Mtu ambaye hana uwezo wa kuamua nani awe mjumbe wa serikali yake ya mtaa, au diwani anawezaje kutunza familia kwa kuingia kwenye ndoa?

Kwa sasa elimu ya msingi na kidato cha kwanza hadi cha nne ni ya lazima kwa watoto wote. Maana yake ni kwamba hawa watakaokuwa shule watalindwa na sheria ya elimu inayozuia mwanafunzi kuolewa na kutoa mwanya wa kumwoza binti ambaye yuko nje ya mfumo wa elimu.

Huu ni ubaguzi wa wazi ambao kamwe haupaswi kufumbiwa macho kwa sababu ya mazingira au hali ya familia. Kwamba wazazi wake wamekosa uelewa wa umuhimu wa shule, basi anakuwa mtu mzima? Hapana.

Ni muhimu ikawepo sheria inayomtafsiri mtoto katika uhalisia bila kujali kama yuko shule au nje ya mfumo wa elimu, bila kujali wazazi wake wana nafasi kubwa au ndogo kiasi gani kwenye jamii.

> **Mtu ambaye hana uwezo wa kuamua nani awe mjumbe wa serikali yake ya mtaa, au diwani anawezaje kutunza familia kwa kuingia kwenye ndoa?**

Ni wazi kwamba mtoto wa mwanasiasa hawezi kuolewa na miaka 18 sembuse hiyo 14, maana yake ni kwamba sheria hii inawaumiza watoto wa masikini ambao mahari inachukuliwa kama chanzo cha utajiri wa familia.

Kumwoa binti wa miaka 14 iwe haramu akiwa shuleni hadi mtaani, kama haruhusiwi kuamua nani awe diwani wake, basi iwekwe wazi kuwa hawezi kutunza mume wala familia.

Ukichunguza waathirika wa ndoa za utotoni, hukuti mtoto wa jaji, hakimu, askari, mwanasiasa, mwalimu wala watu wanaojua umuhimu wa elimu na hatari za kiafya za kubeba jukumu la kulea familia mapema.

Jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba mtoto wa miaka 14 anaolewa na mtu mwenye mara mbili ya umri wake huku wengine wakiolewa na 'babu' zao, hili halikubaliki.

Utakuta watoto wa wafugaji, wakulima wadogo na watu wenye vipato duni ambao wanaona mtoto akipevuka ni mtaji wa kuiondoa familia kwenye lindi la umasikini.

Tumesikia mara kadhaa baadhi ya wazazi wakiwalazimisha watoto wao kufurunda mtihani wa darasa la saba ili wasichaguliwe kuendelea na sekondari, shukrani kwa serikali yetu ambayo imeamua shule ya msingi ni hadi kidato cha nne.

Kama watoto wengi wataingia sekondari, basi watalindwa na sheria ya elimu; hatari na ulazima wa kubadili sheria ya ndoa ni kuhakikisha kwamba mzazi yeyote bila kujali uelewa wake, ana hadhi gani au dunia imempa mtoto taarifa za namna gani, asiolewe chini ya miaka 18.

Tukifanikiwa hapa maana yake ni kwamba tutaweza kupunguza zaidi vifo vitokanavyo na uzazi, udumavu, watoto wanaoishi katika mazingira magumu na ukatili, unyanyasaji majumbani.

## Wahamasisha mkakati kukabili athari mabadiliko ya tabianchi

**Na Zanura Mollel**

BARAZA la Wanawake wa Kifugaji (PWC), limewataka wafugaji na watu wanaoishi pembezoni, kuandaa mpango mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na athari zake kuepukana na maafa.

Ofisa Mradi wa PWC, Rachel Letiety alisema hayo juzi alipotoa mafunzo kwa vijiji vya Wilaya ya Longido vilivyoko kwenye mradi huo.

"Mabadiliko hayo yamechangia athari katika maeneo ya Longido, Monduli na Ngorongoro kwa kupoteza ardhi ya asili.

"Tunasaidia jamii kuotesha nyasi kwenye maeneo yaliyoathiriwa zaidi ikiwamo kwenye nyanda za malisho," alisema.

"Utunzaji wa mazingira pamoja na kutunza vyanzo vya maji ni miongoni mwa njia zinazoweza kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hapa nchini," alisema Rachel.

Alisema wilayani Monduli wanaendelea na upandaji nyasi kwenye nyanda za malisho na wamefanikiwa kupanda ekari 44 katika vijiji vya Selela, Baraka, Losirwa na Makuyuni.

Aidha, kwa Longido mradi huo unatarajia kuwafikia wafugaji 1,550, wanawake 3,000 na wanaume 2,000. "Matarajio ni kuotesha miti kwa kuijenga Longido ya kijani inayoendana na sera ya utunzaji wa mazingira."

Alisema mabadiliko hayo yameonekana kuwaathiri wanawake zaidi na wameanza kutoa mafunzo kwa vikundi vya kinamama 20 katika Wilaya ya Longido na 64 Monduli.

"Kila kikundi tumewawezesha Shilingi milioni moja kwa ajili ya mtaji wa biashara ya pamoja watakayofanya kuepuka kutegemea mifugo katika uendeshaji wa familia kutawasaidia kujikwamu na janga hilo," alisema.

Alisema wamefanikiwa kuwezesha matangi ya kuhifadhia maji ya mvua yatakayosaidia kwenye kilimo cha mboga na matumizi ya kawaida.

"Tumekabidhi matangi 10 Wilaya ya Longido na 24 Monduli kwa kaya zenye uwezo mdogo kiuchumi."

"Wilaya ya Ngorongoro hawajishughulishi na kilimo, tulichoweza kufanya ni kuwapatia chakula kama vile mahindi," alisema.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yamechangia ongezeko la magonjwa ya mlipuko kwa mifugo, pia wamebaini wafugaji kutowapatia chanjo mifugo pamoja na uchafuzi wa mazingira umeonekana chanzo.

Katika hatua nyingine alielezea kuwa nyanda za malisho zinaonekana kupotea kutokana na mabadiliko hayo yaliyochangia mmomonyoko wa ardhi, nyasi kutokuota na kupelekea ongezeko la magugu vamizi.

"Kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu kumechangia mmomonyoko wa udongo na ardhi kutengeneza makorongo yasiyo rasmi," alisema.

Hata hivyo alisema kukosekana kwa miundombinu rafiki ya barabara kumekuwa kikwazo cha mashirika na wadau wengine kuwafikia wananchi kwa wakati.

# SMZ yaiagiza polisi kuharakisha upelelezi ukatili wa kijinsia

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imeliagiza Jeshi la Polisi kuharakisha upelelezi wa kesi za ukatili wa kijinsia ili zimalizwe kwa wakati na kuondoa malalamiko toka kwa wanaotendewa vitendo hivyo.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, katika maadhimisho ya kilele cha siku 16 za harakati za kupinga ukatili na udhalilishaji yaliyofanyika katika Kijiji cha Muyuni, Wilaya ya Kusini Unguja.

Alisema pamoja na kazi kubwa inayofanywa na Jeshi la Polisi, bado ucheleweshwaji wa upelelezi kesi za vitendo hivyo unasababisha kesi nyingi kukaa muda mrefu katika vituo vya polisi.

"Kuendelea kwa mtindo huo kunaweza kuathiri malengo ya serikali ya kupambana na kuondoa vitendo hivyo, kwa hiyo Jeshi la Polisi harakisheni upelelezi wa kesi na kuwatia hatiani wanaothibitika kuhusisha na vitendo hivyo," alisema Rziki.

Alisema, takwimu zinaonyesha kuwa mwaka 2022 kulikuwa na matukio 1,360 yaliyoripotiwa katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, huku 651 kati ya hayo yakiwa ni ya ubakaji, 200 ya ulawiti, 88 kuingilia kinyume na maumbile, 84 kutorosha, 125 kukashifu, na 212 shambulio.

"Wilaya zilizoongoza kwa matukio hayo ni Magharibi A 253, Magharibi B 288 na Mjini 279, pia Januari hadi Oktoba, mwaka huu, kulikuwa na matukio 1,620 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia," alisema.

Alisema ipo haja ya kutambua na kuweka kampeni maalum za kukabiliana na vitendo hivyo ndani ya jamii kwa kuongeza nguvu katika kampeni iitwayo 'Wekeza katika Kuzuia Ukatili Dhidi ya Watu Wenye Ulemavu na Nijuze Nijilinde Dhidi ya Ukatili wa Kijinsia'.

"Usawa kijinsia utakuwa na tafsiri nzuri iwapo kila mtu atatendewa haki kwa mujibu wa sheria, mila na silka za Zanzibar. Nasi kama wizara tumedhamiria kufanya mapitio na kuandaa mpango kazi mpya wa kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto bila kuwasahau na wanaume katika ujumuishaji wa shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2023-2027," alisema.

Awali, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Abeda Rashid Abdalla, alisema bado matukio ya udhalilishaji yanaongezeka ikiwamo kubaka na kunajisi akizitaja wilaya za Mjini na Magharibi B zinaongoza kwa kesi hizo. "Tunapohitimisha kilele cha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia, mapambano bado yanaendelea, hivyo wanaume na wanawake wapambane na vitendo hivyo, kwani bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili viishe," alisema Abeda.

Katibu Tawala Mkoa wa Kusini Unguja, Radhia Rashid Haroub, aliipongeza wizara kwa kuteua mkoa huo kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

"Nguvu zaidi zinahitajika, kwani Mkoa wa Kusini matukio hayo ni mengi, kwani mwaka 2022 yalikuwa 1,320, mwaka huu yameongezeka hadi kufikia 1,620 sawa na ongezeko la asilimia 16," alisema Haroub.

Mkuu huyo wa mkoa aliomba wizara kuja na mkakati utakaoweka misingi mizuri ya kupinga vitendo hivyo hasa katika familia, kwa kuwa matukio mengi ya udhalilishaji yanatokea ndani ya familia.



Mwenyekiti wa Shirikisho la Wenye Viwanda (CTI), Paul Makanza (kushoto), akijadiliana jambo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdalah, wakati wa Mkutano Mkuu wa shirikisho hilo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wakazi Wazo Kota waondokana na kero ya maji

**Na Joseph Mwendapole**

WANANCHI wa Wazo Kota wameondokana na kero ya maji baada ya Mamlaka ya ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), kutekeleza mradi wa maji kwa wakazi takribani 300 wa eneo hilo.

Wananchi wa maeneo hayo awali walikuwa wakipata huduma ya maji kutoka katika kiwanda cha Saruji Twiga kilichopo eneo la Wazo.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, msimamizi wa miradi DAWASA Tegeta, Mhandisi Dominick Mkamba alisema utekelezaji wa mradi umekamilika kwa asilimia 100 na wananchi wanapata huduma ya maji.

"Baada ya kupokea maombi kutoka kwa wakazi wa Wazo Kota, tulianza utekelezaji mara moja, ambao umehusisha ulazaji wa bomba kwa umbali wa kilomita 2.7 ili kuhakikisha wananchi hawa wanapata huduma kwa haraka," alieleza Mhandisi Mkamba.

Aliongeza kuwa ofisi ya DAWASA Tegeta inaendelea na kupokea maombi ya maunganisho mapya ya maji kutoka kwa wananchi wa eneo hilo na kuwasihi kujitokeza kwa wingi kwa kuwa huduma inapatikana.

"Mteja anatakiwa kuwa na vitu vifuatavyo wakati wa kuomba huduma ambavyo ni barua ya utambulisho wa mkazi toka Serikali ya Mtaa anapoishi, picha mbili ndogo, pamoja na nakala ya kitambulisho cha taifa au kitambulisho cha mpiga kura, leseni ya gari au hati ya kusafiria," alisema Mkamba.

Mkazi wa eneo hilo, Apolonia Kagaruki aliishukuru DAWASA kwa kufanyia kazi maombi yao kwa wakati na sasa wanafurahia huduma ya maji.

"Awali hatukuwa na huduma ya DAWASA, maji tuliyoyatumia kutoka kiwanda cha Saruji Wazo yalikuwa na chumvi nyingi na hivyo kusababisha tuyatumie kwa matumizi ya majumbani zaidi na tununue ya kwenye magari kwa matumizi ya kibinadamu kama vile kupikia," alisema.

Mradi wa maji Wazo Kota unagharimu Shilingi Milioni 26.2 utahudumia wakazi zaidi ya 300 eneo la Wazo Kota na mtaa wa Kilembela watakaopata huduma bora na yakutosheleza wakati wote.

# Maneno ya waziri nusura yamlize diwani

**Na Munir Shemweta,** SINGIDA

MANENO ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geoffrey Pinda, wakati wa kutafuta suluhu ya mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kisaki na mwekezaji katika eneo la Kisaki B, Manispaa ya Singida, nusura yamlize Diwani wa Kisaki, Moses Shaban, kutokana na kujaa hekima na busara.

Naibu Waziri Pinda alifika kijiji cha Kisaki kilichoko mpakani mwa Manispaa ya Singida na wilaya ya Ikungi mkoani Singida juzi kwa lengo la kusikiliza na kutatua mgogoro wa ardhi baina ya wananchi na mwekezaji wa ufugaji nyuki.

"Nikupongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Naweza kusema hata kama hatujafika mwisho wa jambo hili, umenipa hadidu za rejea kumkumbuka Mizengo Pinda alipokuwa Waziri Mkuu kuhusu hekima yake na maelekezo yake juu ya utendaji kazi.

"Nilikuwa nimesimama na kukusikiliza natamani kulia kwa sababu umekuja katika mgogoro huu hakika umeiwakilisha vyema serikali," alisema.

Diwani huyo alisema maneno yaliyozungumzwa na Naibu Waziri Pinda kuhusu utatuzi wa mgogoro baina ya wananchi na mwekezaji ni tunu yenye afya na mbolea katika kutatua mgogoro wa ardhi katika eneo hilo.

"Umeongoza kikao kilaini na kitamu hata aliyekuwa na hasira zimepotea na hata yule aliyekuwa na silaha ameshusha, nakupongeza sana," aliongeza diwani huyo.

Naibu Waziri Pinda aliwataka wananchi wa Kisaki kudumisha amani katika muda wote wa kushughulikia migogoro ya ardhi kwenye maeneo yao.

"Niwatangazie kipande cha amani wote bila kujali ukoo wa nani na muwe na lugha moja iliyo bora. Siri ya mgongano inapata adui anayeingia bila matatizo," alisema.

Pia aliwataka wananchi wa kijiji cha Kisaki kwenda kuanza vikao vya suluhu ya mgogoro wao na suala la kukutana na serikali basi ofisi ya mkuu wa wilaya ya Singida italisimamia kwa kuwa suala hilo lishatoka katika ngazi ya kijiji.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskasi Muragili, alisema mgogoro wa ardhi baina ya wananchi wa kijiji cha Kisaki na mwekezaji katika eneo la Kisaki B, ulifika ofisini kwake mwaka 2022 na wananchi walidai maeneo kutwaliwa na mwekezaji.

Hata hivyo, alisema kutokana na kadhia hiyo aliunda timu kubaini kama madai ni ya kweli au la na timu hiyo ilimaliza kazi Mei, mwaka huu na kupeleka mrejesho katika ofisi yake Oktoba, mwaka huu.



Wajumbe wa Taasisi ya Nipael Foundation iliyoanzishwa kwa kusudi la kutumia ubunifu na sanaa katika kusaidia jamii kukabiliana na changamoto mbalimbali ili kutoa elimu, misaada na fursa kwa kuleta maendeleo, kuinua na kukuza uchumi kwa kuzingatia makundi maalum. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanaojifungua watoto njiti kuongezewa likizo

**Na Frank Monyo**

CHAMA cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE), kimetia saini mkataba wa hali bora na watumishi wake unaolenga kuboresha maslahi yao katika maeneo mbalimbali.

Akizungumza jana baada ya kusainiwa kwa mkataba huo, Katibu Mkuu wa TUGHE, Hery Mkunda, alisema kwa mara ya kwanza mkataba umeongeza idadi ya siku ya likizo kwa mfanyakazi mwanamke atakayejifungua mtoto njiti na kufanya TUGHE kuwa chama cha kwanza kuweka kipengele hicho katika mkataba wake wa Hali Bora.

Mkunda alisema lengo la kuboresha kipengele hicho ni kutambua na kuthamini mchango mkubwa unaofanywa na wanawake ndani ya TUGHE kitendo kitakachoongeza tija na ufanisi ndani ya chama.

Aidha, aliiomba serikali kupitia upya na kuboresha sera na sheria mbalimbali zitakazojumuisha wanawake wanaojifungua watoto njiti kama TUGHE ilivyoanza kufanya ili kuwapatia muda wa kuwahudumia watoto pamoja na kuimarisha afya zao.

Makamu Mwenyekiti wa TUGHE, Dk. Jane Madete, alisema amefurahishwa na uamuzi huo wa kufikia makubaliano hayo kati ya uongozi na wafanyakazi kwa kuwa utaenda kuongeza ari ya kufanya kazi kwa bidii na kukifanya chama kipige hatua mbele zaidi.

Viongozi wa tawi la TUGHE kwa niaba ya wafanyakazi walisema, wamefurahishwa na mkataba huo ambao umegusa maeneo yote muhimu ambayo kwa muda mrefu walikuwa wanaomba uongozi uyafanyie maboresho.

Mkataba uliosainiwa ni wa muda wa miaka mitatu na una kipengele cha kufanyika kwa marekebisho muda wowote na pande zote mbili zitaona kuna uhitaji wa kufanya hivyo. Pia mkataba huo utawahusu wafanyakazi wote walio katika ajira ya kudumu na mikataba ya muda maalumu na chama.

# Waziri kuongoza harambee kuchangia watoto wahitaji 5,000

**Na Henry Mwangonde**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, anatarajia kuwa mgeni rasmi kwenye harambee ya kuchangia sare kwa watoto wenye uhitaji, ikiwa na lengo la kuwafikia watoto 5,000.

Harambee hiyo imeandaliwa na mbunifu wa mavazi, Ruth Urio na itafanyika Desemba 16, mwaka huu, jijini Dar es Salaam kwa lengo la kutafuta fedha.

Katika harambee hiyo, kutakuwa na maonyesho ya mavazi na mapato yatatumika kununua sare hizo.

Urio ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Jadore Couture, alisema tukio hilo litahusisha uuzaji wa bidhaa za mitindo.

"Lengo ni kurudisha kwa jamii na tunaamini kuwa tukio hili litakuwa na matokeo chanya kwa walengwa, hivyo tunawaalika wadau mbalimbali kushiriki nasi," alisema.

Alisema wazo hilo lilitokana na ukweli kwamba licha ya jitihada nyingi za kuboresha elimu, bado wanafunzi wengi wanakosa mahitaji maalumu, ikiwamo sare.



Tukio hilo, alisema linalenga kuwafikiwa wanafunzi kati ya 1,000 hadi 5,000 na kwamba, wamekuwa wakifanya matukio kama hayo na mwaka huu ukiwa ni wa tano.

Hivi karibuni serikali imefanya maboresho kwenye baadhi ya maeneo katika Sera ya Elimu na Mafunzo ili kutoa elimu ya ujuzi badala ya elimu ya taaluma pekee ambapo elimu ya lazima itakuwa ya miaka 10 badala ya saba kama ilivyo sasa.





## Kanisa lakabidhi milioni 22/- waathirika maafa Hanang'

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

KANISA la Waadventista wa Sabato kutoka Jimbo Kuu la Kaskazini mwa Tanzania, limekabidhi Sh. milioni 22. 5 kwa serikali, kwa ajili ya kusaidia waathirika wa maafa ya maporomoko ya tope, mawe na magogo yaliyosababisha vifo vya watu 87 na kujeruhi wengine 116 katika Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara.

Askofu Mkuu wa Jimbo hilo, Mch. Mark Malekana, Akizungumza jana kabla ya makabidhiano hayo, alisema kanisa hilo linatoa pole kwa waathirika wote na wataendelea kuwaombea, kwa kuwa jamii hiyo inahitaji misaada mbalimbali ikiwemo ya kiroho.

"Kanisa limeguswa sana na maafa haya na tunaungana na serikali kutoa pole na kwa leo, tunakabidhi Sh. milioni 22.5 ambazo zitasaidia kuendelea kurejesha hali kwa wenzetu waliofikwa na maafa haya," alisema Askofu Malekana.

Alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kusimamia suala hilo na kulipa uzito unaotakiwa kwa kuhakikisha viongozi wa serikali wanaratibu na kushughulikia kwa ufanisi mkubwa ili kuwapa unafuu waliofikwa na maafa hayo.

"Serikali mmefanya kazi kubwa na mnaifanya usiku na mchana, Kanisa limeona liungane nanyi ikiwa ni sehemu ndogo tu, tunaahidi kuendelea kufanya zaidi kadiri Mungu anavyotubariki ili kuwapa faraja na nguvu ndugu zetu waliopata maafa," alieleza.

Baada ya makabidhiano hayo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Dk. Jim Yonazi, alilishukuru kwa kujitoa kifedha na kiroho huku akiahidi kuwa fedha zote zinazotolewa zitawafikia walengwa na kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa.

"Kanisa la Waadiventista wa Sabato tunawashukuru kwa kuendelea kutuombea naamini kwa namna mlivyojitoa leo ni jambo la baraka sana kwao na familia zao kwa ujumla kwa kuzingatia wamewapoteza wapendwa wao, niwaombe msiache kuwaombea kila siku ili Mungu aendelee kuwapa amani na furaha katika wakati wanaopitia," alisema Dk. Yonazi.

# Wavamizi wa msitu hifadhi wapewa siku 18 kuondoka

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

SERIKALI imewapa siku 18 wananchi wa vijiji vya Nadare, Losirwa na Ilorienito, waliovamia Msitu wa Hifadhi wa Mlima Ketumbeine, ulioko Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, kuondoka kwa hiari, badala ya kusubiri matumizi ya nguvu.

Wananchi hao ambao ni wafugaji wa jamii ya Kimasai, wanadaiwa kuharibu vyanzo vya maji na kuhujumu shughuli za uhifadhi wa msitu huo kwa kuendesha shughuli za kilimo, kujenga makazi, kukata miti ovyo na kuchungia mifugo ndani ya vyanzo vya maji.

Wakati amri hiyo ya kuondoka ikikaribia ukingoni, Shirika la Kimataifa la World Wide Fund (WWF), limelazimika kuendesha kampeni ya kurejesha uoto wa asili katika msitu huo wa hifadhi, kwa kupanda miti.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Marko Ng'umbi alisema: "Disemba 30, mwaka huu, watu wote waliovamia msituni wawe wameondoka. Niliwapa miezi mitatu, maboma yote yaondoke. Tulikubaliana hivyo pale Kijijini Losirwa kwenye mkutano, pale Ilorienito na pale Nadale; tukakubaliana hivyo pale Njoro, kule Sokoni na tukakubaliana hivyo kwenye mkutano pale Langa'ta Dabashi.

"Nilisema ondokeni kwa hiari yenu, na ndio maana mmepewa muda wa kujiandaa kuondoka mrudi upande wa pili. Huko mnakorudi ni huruma ya serikali.

...Leo nazungumza kama mchungaji wa Kipentekoste hivi, nitakaporudi na Kanisa langu la Pentekoste moto moto, mtaelewa sasa kwamba hali itakuwaje."

"Ukweli ni kwamba hali ya msitu wetu ni mbaya. Ni mbaya kwa sababu watu wamevamia kwenye vyanzo vya maji, watu wameingia kulima msituni. Ni mbaya kwa sababu watu wanakata miti, watu wameanzisha makazi, ni mbaya sana kwa sababu watu wanaingiza mifugo mpaka juu kabisa viliko vyanzo vya maji."

Meneja wa Mradi Land for Life, Reguli Marandu, akizungumzia kampeni hiyo alisema:

"Tumekuwa tukifanya kazi za uhifadhi katika vijiji vyenu, na tukisema uhifadhi tunaangalia uhifadhi wa mazingira, tunaangalia uhifadhi wa wanyamapori lakini tunaangalia namna gani uhifadhi, unasaidia jamii zile zinazozunguka hayo mazingira, ambayo tunayahifadhi.

"Dhana ya WWF, tunataka jamii zile zinazoishi kwenye hayo mazingira pamoja na wanyamapori na mazingira yetu, vyote viwe vina ustawi ambao ni mzuri.

...Kwa hiyo tuliona ni vizuri siku ya leo ambayo ni maadhimisho ya Uhuru wa Tanganyika, tumuunge mkono Mkuu wa Wilaya kufanya kazi ya upandaji miti kwa ajili ya kutunza vyanzo yetu vya maji. Ninyi wananchi wa Ilorienito hapa mlipo mnashikilia ustawi wa watu wengi, kuna vijiji vingi viko bondeni hawana vyanzo vya maji Na wanategemea chanzo hiki cha maji ili waweze kupata maji.

"Tunawajibu kama wakazi wa kata hii kuhakikisha tunatunza msitu ambao unazunguka vyanzo vya maji. Tumewawezesha kufanya kilimo cha alizeti, mkikosa maji mtalima alizeti? Haya yote ni kwa ajili ya kuwawezesha kuongeza kipato.

"Ni jukumu letu sisi ambao tunakaa karibu na vyanzo vya maji, tuwe sehemu ya uhifadhi na ukimuona mtu anakata miti unatakiwa utoe taarifa kwenye kamati ya ulinzi ya kijiji chenu. Namuahidi Mkuu wa Wilaya kwamba tutaongeza, tutaleta miti mingine tena kama 500."

Diwani wa Kata ya Ilorienito, Sano Otusu, aliwahadharisha wakazi wa vijiji hivyo kuwa, hakuwaomba kura ili aje awaruhusu kwenda kuishi ndani ya msitu.

"Naomba niwaambie ukweli, msitu ni msitu na maeneo ya kilimo ni ya kilimo, mkae mkijua hilo kwamba serikali ina dhamira njema sana kupanda miti ili kuokoa misitu yetu isije ikatoweka.

"Sikuwaomba kura ili niwaruhusu kwenda kuishi ndani ya misitu, nilisema nakwenda kuwasaidia kuleta miradi na ndio mradi ambao naupambania kisiasa, maji yapo, umeme, barabara na kadhalika."

Msitu wa Hifadhi wa Ketumbeine, ulitangazwa kuwa eneo la msitu wa hifadhi ya Mlima Ketumbeine mwaka 1958.




Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Mahusiano ya Umma wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu (wa pili kushoto), akiwaongoza wafanyakazi wenzake kushusha shehena ya msaada wa mahitaji ya kibinadamu ikiwemo chakula, nguo na mablanketi vyenye thamani ya sh. milioni 20, kabla ya kukabidhi kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jimmy Yonaz (kushoto), wilayani Hanang, mkoani Manyara jana, kwa ajili ya wahanga wa mafuriko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hofu Mlima Kilimanjaro kutoweka barafu 2050

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imeeleza hofu yake kuhusu kutoweka kwa barafu ya Mlima Kilimanjaro ifikapo mwaka 2050, kutokana na kutishiwa na majanga ya mioto, ujangili wa mazao ya misitu na shughuli za kiuchumi.

Hatari hiyo inachagizwa na shughuli zinazofanywa na wananchi wa vijiji vinavyouzunguka mlima huo kutoka Wilaya nne za Hai, Siha, Rombo na Moshi na baadhi ya sehemu ya ukanda wa Pwani.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Anjelah Kairuki, aliyasema hayo juzi, wakati wa hafla ya kuwapokea wazalendo 208 waliokwenda kusheharekea sherehe za uhuru wa Tanganyika katika kilele cha Uhuru, chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari.

Alisema jitihada zaidi kutunza mazingira kwa kupanda miti ili kulinda barafu ya Mlima Kilimanjaro kutokana na ikolojia ya mlima huo mrefu kuliko yote barani Afrika kuendelea kupungua kutoka tishio la shughuli za kiuchumi.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Uendeshaji wa Shughuli za Utalii ya ZARA Tours, Zainab Ansel, alisema kampeni ya Twenzetu Kileleni, imewapa uzoefu mkubwa wa kujua kitu gani cha kufanya, na ni kitu gani cha kujivunia, baada ya kufanikiwa kushawishi wageni 208 kupanda kupitia kampeni hiyo.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kampeni hii ya Twenzetu Kileleni na kuitangaza Tanzania nje ya nchi kupitia Filamu ya 'The Royal Tour' kwa sababu sasa watalii wanajua Mlima Kilimanjaro uko wapi.

"Tunawashukuru Wizara ya Maliasili na Utalii na Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Jenerali Mstaafu, George Waitara, kwa kuendesha kampeni hii ya mafanikio kwa miaka 15 sasa."

Aidha, Mkurugenzi wa Kampuni ya African Scenic Safaris, Simbo Natai, alisema wanashukuru kwa kuaminiwa na serikali na kupewa njia mpya ya Lemosho (Siha), ambayo ni kwa mara ya kwanza, inapeleka Watanzania kileleni kusherehekea miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika.

"Njia hii ni mahususi kwa sababu ndio njia bora ya kupanda Mlima Kilimanjaro, utaona kwamba wale wote waliopita njia ya Lemosho wote wamefika kilele cha Uhuru na wamerudi salama,"alisema Simbo.



# RC aitaka polisi kuingilia kati ukeketaji Mara

**Na Timothy Itembe,** MARA

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yaya Newanda, amelitaka Jeshi la Polisi Mkoa wa kipolisi Tarime/ Rorya, kuingilia kati vitendo vya ukeketaji wa watoto kwa kuwakamata na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria wahusika wa vitendo hivyo.

Dk. Newanda alitoa rai hiyo juzi katika kilele cha maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili na kulitaja jeshi hilo kuwa na nafasi kubwa ya kukabiliana na vitendo hivyo.

Alisema jeshi linatakiwa kuwakamata wale wote ambao wanaendelea kufanya vitendo hivyo vya kikatili dhidi ya watoto wa kike na hatua hiyo iwe fundisho kwa wengine.

"Ukeketaji hauna nafasi kwenye karne hii na ni hatari unatakiwa kukomeshwa mara moja kwani ni ukiukwaji wa haki za binadamu na watoto hivyo Jeshi letu liwe msaada kukabiliana na vitendo hivi kwa kushirikiana na wadau wengine," alisema Newanda.

Meneja Mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko alisema, wanashirikiana na serikali kuhakikisha sheria zinazomlinda mtoto wa kike zinatekelezwa.

Mkurugenzi wa halmashauri ya Tarime, Solomon Shati alisema hali ya ukatili kwa miaka mitatu 2022 hadi 2023 ni 9,284 wanaume 1,611 na wanawake 7,673 na kutaja ukatili huo kuwa kikwazo kwa maendeleo.

"Kama halmashauri tunatekeleza sera, miongozo, sheria na kanuni mbalimbali katika kulinda na kusimamia haki na ustawi wa mtoto, vijana, wanawake, wazee na watu wenye ulemavu pampja na makundi yote yenye uhitaji," alisema Shati.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme (katikati), akikata utepe ikiwa ishara ya kuwasha umeme katika vijiji 17 kati ya 46 vya Halmashauri ya Ushetu, Kijiji cha Zobogo, Kata ya Igunda jana, akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita na wa pili kulia ni Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani na wananchi wa kijiji hicho. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wajenga kituo cha polisi kudhibiti uhalifu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Ulowa, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wamelazimika kuchangishana fedha na kujenga kituo cha polisi ili kukabiliana na hali ya uhalifu iliyokithiri katika eneo hilo.

Kata hiyo inatajwa kuwa na vitendo vya uvunjifu wa amani ikiwa ni pamoja na uvunjaji wa maduka ya biashara, makazi pamoja na wizi wa mifugo hasa ng'ombe. Katika kukabiliana na vitendo hivyo wananchi wa kata hiyo walichangishana kila kaya ili kufanikisha ujenzi wa kituo hicho ambao unaendelea chini ya Kamati ya Maendeleo ya kata kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mkoa.

Diwani wa Kata hiyo, Gabriela Kimaro, akizungumza juzi wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo, alisema kutokana na vitendo hivyo iliwalazimu polisi kukodi nyumba kwa gharama ya Sh. 150,000 kwa mwezi na kuweka kituo cha polisi cha muda.

Alisema, kwa wiki walikuwa wakivamiwa mara mbili hali iliyofanya kukutana na kujadili namna ya kujenga kituo cha polisi ili kudhibiti tatizo hilo na mwaka 2019 serikali ya Kijiji cha Kangeme ilitenga eneo lenye ukubwa wa hekari moja na kuanzisha ujenzi kwa Shilingi milioni saba zilizokuwa zimepatikana kwenye mchango na jeshi la polisi lilitoa mchoro wa ramani ya jengo linavyotakiwa kuwa na sasa lipo katika hatua ya mwisho ya ukamilishaji.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shanyanga, Janeth Magomi, aliwapongeza wananchi kwa kuanzisha ujenzi huo kwa gharama zao kwa kuwa awali walilazimika kutembea umbali wa kilometa 45 hadi kituo kikubwa cha polisi Nyamilangano kupata huduma, na kumshukuru mkurugenzi kwa kutoa Sh.milioni 20 za ukamilishaji ili waondoke kwenye jengo la kupanga.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, aliwataka wananchi wa kata nyingine zenye kero za uhalifu kuinga mfano huo na kuacha kusubiria serikali kufanya kila kitu kwani maendeleo yanaletwa na wananchi wenyewe kulingana na uhitaji wa jambo wanalolihitaji nasio vinginevyo.

Aidha, alichangia Shilingi milioni moja na kuitaka kamati ya ujenzi kusimamia kwa kuzingatia viwango vinavyohitaji na kumwagiza Mkandarasi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) kufikisha umeme katika kituo hicho mapema iwezekanavyo.

## 'Smart' kuanza na miradi ya chama iliyotelekezwa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

MWENYEKITI wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mwanza, Michael Lushinge, maarufu 'Smart' ameonesha nia ya kufufua na kuboresha miradi ya chama hicho iliyotelekezwa ukiwamo uwanja wa mpira wa CCM Kirumba.

Lushinge alitoa ahadi hiyo juzi mbele ya wanachama wa mkoa wakati akikaribishwa baada ya kushinda wadhifa huo hivi karibuni akichukua nafasi ya Sixberth Jichabu aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

Alisema uboreshaji wa miradi hiyo utakuwa ni miongoni mwa jitahada muhimu za kuinua vitega uchumi vya chama hicho na kuleta maendeleo katika jiji la Mwanza.

"Mwanza ni mkoa wa kimkakati na tuna miundombinu mingi ikiwamo uwanja wetu wa Kirumba lazima tuiboreshe kwa maslahi ya chama na mkoa nitauwekea taa ili sisi wana Mwanza na Kanda ya Ziwa tufurahie michezo ya usiku," alisema.

"Vilevile, lazima tuongeze miradi mipya ya chama pia bila kusahau miradi yote ya kimkakati inayotekelezwa na serikali niahidi kwenda kusimamia ili kuleta tija kwa chama na serikali," alisema Lushinge.

Aidha, aliwata wana CCM kushikamana kwaajili ya kutekeleza malengo ya serikali kwa wananchi lengo likiwa ni kufikia uchaguzi wa 2024 na 2025 wakiwa na kauli moja kwa wananchi na kuibuka kidedea.

Mwenyekiti huyo licha ya kuwataka waliokuwa wagombea wenza kutoa ushirikiano wa karibu katika utekelezaji wake wa majukumu ya chama alitoa vyeti vya heshima kwa wagombea hao zaidi ya 100 na kuwata waendelee kuwa wamoja ili kukijenga chama na kuwatumikia wananchi.

Mjumbe wa NEC Mkoa wa Mwanza, Jamali Abdul, aliwataka wanachama hao kuvunja makundi yao ya awali ya uchaguzi ili kujiandaa na uchaguzi wa serikali za mitaa ikiwa ni pamoja na uchaguzi mkuu.

"Wapo viongozi wanajiona ni miungu watu wanafanya mambo kinyume na taratibu za chama na kushindwa kuwapa nafasi watu wenye uwezo wa kuongoza waliopo huko katika ngazi za matawi bali wanawapa watu wasiokubalika na wananchi ili kufanikisha mambo yao binafsi hatutawavumilia," alisema Jamali.

**Alisema uboreshaji wa miradi hiyo utakuwa ni miongoni mwa jitahada muhimu za kuinua vitega uchumi vya chama hicho na kuleta maendeleo katika jiji la Mwanza.**



Ukurasa 12

**Fagio la Mwinyi mahakamani mrundikano kesi wawa historia**



Ukurasa 13

Watetezi wa haki wajikumbuka, waanzisha kituo cha kujiganga


# siasa

JUMATANO DESEMBA 13, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 14

**TSHISEKEDI VS KATUMBI**

**Uasi wa M23 unavyotishia hatima ya Rais kurejea Ikulu**

MIAKA 75 TAMKO LA HAKI

# AZAKI zina jambo lao uhuru kamili, zachoka kubinywa, sheria mbovu

**Na Sabato Kasika**

WATETEZI wa haki za binadamu, wanakutana kurejea miaka 75 ya Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu, lililozaliwa mwaka 1948.

Kusanyiko la maadhimisho ya miaka 75 linalofanyika Dar es Salaam, linaziibua Asasi za Kiraia (AZAKI), zinazosema zinatamani kupewa uhuru wa kufanya kazi bila kuingiliwa.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), ndicho mratibu wa kongamano, kikishirikisha wadau mbalimbali wakiwamo majaji wastaafu, wanasheria, viongozi wa kisiasa na asasi za kiraia.

Katika mdahalo, Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa LHRC, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema AZAKI zimeminywa, mashirika watetezi nayo yameshindwa kujitetea na kubaki kimya.

"Mabadiliko ya sheria ya AZAKI yameathiri mno shughuli zetu tofauti na tulivyokuwa tukitekeleza majukumu haya miaka ya 1990," anakumbusha Dk. Hellen.

Aidha, anaongeza kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya ili sheria ya AZAKI ibadilishwe na kuwapa uhuru wa kutekeleza majukumu ya kusaidia serikali bila kuingiliwa.

"Ninasema hivyo, kwa sababu sisi ni wadau ambao tunaisaidia serikali kutunga sheria. Watu wanapokwenda katika mikutano ya kimataifa kuzungumzia haki za binadamu, sio siri kwamba mara nyingi taarifa zetu huwa ni nzuri tu," anasema.

Aidha, anaongeza kuwa hatua ya kuingizwa haki za binadamu kwenye katiba, inatokana na harakati zilizofanywa na watu mbalimbali miaka 75 iliyopita, na kwamba hata Tanzania imeridhia mikataba mingi na kwamba hilo ni jambo jema.

"Kimsingi, taifa lilijiunga katika Tamko la Haki za Binadamu mara baada ya kupata uhuru, wakati huo hatukuwa na mifumo mizuri ya usimamizi wa haki za binadamu," anakumbusha.

Baada ya uhuru kulikuwa na vyombo vya habari viwili vya serikali, baadaye redio zikaanza kuongezeka ndipo nao wakapata fursa ya kuzungumza haki za binadamu na kuanza kuridhia matamko mbalimbali ya haki za binadamu, anaeleza Dk. Hellen.

"Lakini pamoja na hayo, kuna wakati fulani haki za binadamu zilikuwa hazitekelezwi inavyotakiwa. Ilifika kipindi haki za kisiasa ziliminywa pasipo kufuata katiba, bali tamko la kuzuia mikutano ya vyama vya siasa, kuminywa uhuru wa vyombo vya habari," anakumbusha.

**MKANGANYIKO**

Wakili wa Mahakama Kuu, Bahame Nyanduga, anasema kuna changamoto kubwa ya uelewa wa haki za binadamu na ikitokea mtu anazipambania, huitwa mwanaharakati.

"Hii ni dhana mbaya, tutambue kuwa haki za binadamu ni za kila mtu, hivyo si sahihi anayepambania kuitwa mwanaharakati," anaonya Nyanduga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, Rebeca Gyumi, anasema, baada ya kutungwa Sheria ya Mtoto ya 2009 kuna baadhi ya haki wameanza kuzipata lakini bado kuna ubaguzi wanaupitia na kwamba sheria ya haki ya mtoto inakinzana na kusababisha wakose haki zao nyingine.

"Pamoja na hayo anawasifu wanawake wamekuwa vuguvugu la harakati za kupambania haki zao, tumeoma ujio wa mashirika mengi yaliyofunguliwa baada ya Mkutano wa Beijing 1995," anasema Rebecca.

Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji Matthew Mhina, anasema, ni muhimu kutatua baadhi ya changamoto ambazo zinachangia kuwapo kwa ukiukwaji wa haki za binadamu, ili kuendelea kuzilinda.

"Kuna hatua zilizofikiwa na Tanzania kutetea haki za binadamu, ikiwamo kuwa na vituo vya usimamizi wa haki, uwepo wa mashirika ya kijamii ya utetezi wa haki na serikali kupitia vyombo vya usalama wa raia," anasema Jaji Mhina.



Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa LHRC, Dk. Hellen Kijo-Bisimba. **PICHA: TAMWA**

Anaongeza kuwa katika kulinda haki za binadamu, ni vyema kila mmoja kwa nafasi yake ahusike. Mwakilishi Mkazi Kanda ya Afrika, Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu, Marcel Akpovo, anaomba serikali kurudi kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Haki za Watu.

"Niipongeze Tanzania kwa kuuridhia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa, ila ninaiomba irejeshe uanachama wa mahakama hiyo, ni muhimu kwa utekelezaji wa haki za binadamu," anasema Akpovo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, anatoa wito kwa serikali kusimamia kukamilifu haki za binadamu ili kufikia maendeleo endelevu.

Aidha, anasema watu wengi duniani bado wanakabiliwa na changamoto kutokana na ukiukwaji na kutozingatiwa kwa haki za binadamu, watu bilioni 2 wanaishi wana njaa, umaskini wa kutisha.

"Tumefanya tafakari na kubaini kuwa sababu kuu ni kwamba malengo 17 ya maendeleo endelevu hayatekelezwi ipasavyo, hivyo nitoe wito kwa serikali kuendelea kusimamia haki za binadamu," anasema Dk. Anna.

Mkurugenzi Mtendaji huyo anafafanua kuwa lengo namba moja la maendeleo endelevu ni kushughulikia umaskini, lakini watu bado wanaishi katika umaskini mkubwa.

"Kwa Tanzania, zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni maskini, ni asilimia 20 tu wanaoishi katika tabaka la kati na la juu la jamii, hivyo hii bado ni changamoto kubwa," anasema.

Anasema kuna makundi mengi ambayo haki zao zinaminywa akifafanua kuwa asilimia 47 ya vitendo vyote vya ukiukwaji wa haki za binadamu vinagusa watoto, kundi la pili likiwa ni wanawake, na kwamba asilimia 33 ya uhalifu dhidi ya haki za binadamu unawapata wao.

# Fagio la Mwinyi mahakamani mrundikano kesi wawa historia



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimwapisha Jaji Mkuu wa Zanzibar, Khamis Abdallah Ramadhan. **PICHA: IKULU**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MIAKA mitatu ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ikulu, imetoa majawabu ya kero sugu nyingi zikiwamo za muhimili wa mahakama moja ya nguzo muhimu katika kutoa na kusimamia haki, ulikuwa ukishtumiwa kwa mrundikano wa kesi za jinai.

Mahakama yenye jukumu la kutafsiri sheria na kutoa haki iwe kwenye makosa ya jinai au ya madai, ililalamikiwa na wengi. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, mamlaka ya kutoa haki yatakuwa mikononi mwa Idara ya Mahakama.

Akizungumza na Nipashe kuhusu mafanikio ya muhimili huo wa Mahakama Zanzibar katika miaka mitatu ya Rais Mwinyi, Jaji Mkuu wa Zanzibar Khamis Abdallah Ramadhan, kubwa ni kuendesha kesi kwa ufanisi pamoja na kupunguza muda wa kusikilizwa na kutolewa hukumu husus an za jinai.

Anasema mashauri ya jinai yanachukuwa wastani wa miezi sita kumalizika tangu kufunguliwa mahakamani akiongeza: "Mheshimiwa Rais ni muumini wa mabadiliko katika mahakama na kabla ya uongozi wake kulikuwa na changamoto nyingi sana na ameanza kutatua ikiwamo kuendesha mashauri hasa ya udhalilishaji kwa muda mrefu mno," anasema.

Moja ya utatuzi wa changamoto hiyo ni kuchagua mahakimu maalum wa kusikiliza mashauri ya kesi za udhalilishaji na dawa za kulevya katika kila mkoa, anasema Jaji Mkuu.

Hatua hiyo imesaidia mashauri mengi kumalizika kwa kasi kiasi ambacho uhai wa mashauri ya dawa za kulevya au udhalilishaji husikilizwa kwa muda usiozidi miezi sita, anaongeza.

> Imefikia kiasi ambacho hata washtakiwa wa kesi hizo wanajiuliza mbona kesi inapangwa na kusikilizwa mara kwa mara? Pemba mashauri ya kesi hizo yamemalizika na yaliopo hayazidi matano kwa kesi za udhalilishaji.

"Imefikia kiasi ambacho hata washtakiwa wa kesi hizo wanajiuliza mbona kesi inapangwa na kusikilizwa mara kwa mara? Pemba mashauri ya kesi hizo yamemalizika na yaliopo hayazidi matano kwa kesi za udhalilishaji," anasema.

Aidha, anasema katika mahakama kuu, hivi sasa mashauri ya dawa za kulevya yenye kiwango kikubwa ambacho kimetajwa katika sheria ndio hufikishwa mahakama kuu na kasi ya usikilizaji imeongezeka.

Jaji Mkuu, anasema kuna mashauri ya rushwa na uhujumu uchumi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa yanachelewa kusikilizwa lakini tatizo lipo katika sheria hivyo wameshatengeneza rasimu ya mswaada wa mahakama maalum ya rushwa na uhujumu uchumi na rasimu hiyo ikipita katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar itakuwa na mahakama maalum ya rushwa na uhujumu uchumi.

Anasema uwepo wa mahakama hiyo mashauri ya rushwa na uhujumu uchumi yatasikilizwa kwa haraka kwa sababu kwa sasa kuna mkwamo, mashauri yanapofika mahakamani jaji anayepangiwa huwa na mchanganyiko wa kesi nyingi zikiwamo za jinai na madai.

"Tatizo kubwa tunalolipata ni kuyarundika mashauri ya aina moja katika mahakama moja, unapoamua kusema mashauri ya dawa za kulevya yasikilizwe katika mahakama kuu peke yake ilo linakuwa tatizo lazima mamlaka ya usikilizaji wa mashauri yashuke katika mahakama zote ili kutozinyima nyingine kutokuwa na mashauri ya kusikiliza," anasema.

Kadhalika, ucheleweshaji wa kusikiliza mashauri unachangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo baadhi ya wadau kuchelewesha usikilizaji wa kesi mfano jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Malaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ingawa kwa sasa wanafanya kazi kwa ushirikiano na mkwamo huo umeondoka.

"Kwa kiasi fulani tatizo lipo lakini halitokani na mahakama peke yake bali kuna wadau mbalimbali kama vile DPP, Jeshi la Polisi, mawakili wanapelekea kuchelewa kusikilizwa kwa kesi kwa mfano mashahidi kutofika mahakamani na dharura za mawakili," anasema.

Jaji Mkuu anasema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dk. Mwinyi serikali, ilitoa idhini kwa Mahakama Kuu kuajiri watumishi wapya hali ambayo imeongeza ufanisi.

Sambamba na uwepo wa jengo jipya la Mahakama Kuu, serikali imeanza na ujenzi wa mahakama za wilaya na mikoa Unguja na Pemba.

Anasema kwa mara ya kwanza alipochaguliwa kuwa Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar kipaumbele chake kilikuwa kuleta maboresho ya mahakama kwa lengo la kuwaondoshea kero wananchi.

"Katika kulitekeleza hilo kwa vitendo niliunda kamati tano za maboresho kwa kunishauri mambo yanayohitajika katika mihimili ya mahakama ambapo kamati hizo ni ya maboresho, mafunzo,usimamizi, ufuatiliaji na tathmini, kamati ya kanuni, takwimu na TEHAMA,"anasema Jaji Ramadhan.

Akizungumza kuhusu mafanikio ya kupunguza kesi za udhalilishaji mahakamani, jaji huyo anasema mahakama imejiwekea mikakati ya kuzipunguza kesi za udhalilishaji kwa kuanzishwa mahakama maalumu kuzisikiliza na kuzitolea uamuzi kwa haraka.

"Sasa niseme kuwa ingawa tatizo hili halijaisha lakini hivi sasa wana jamii wengi wamekuwa na hofu kubwa ya kutenda makosa ya udhalilishaji kutokana na adhabu kali zinazotolewa mahakamani." Anasema Jaji Mkuu.

**MSONGAMANO**

Anazungumzia msongamano wa mahabusu gerezani, akisema tatizo hilo linasababishwa na uwepo wa sheria nyingi ambazo zinawanyima dhamana washtakiwa wa makosa ya udhalilishaji na dawa za kulevya.

Anashauri kuwa katika kupunguza tatizo hilo la mrundikano wa mahabusu gerezani kuna haja ya kuzipitia tena sheria ili kuona uwezekano wa kuweka dhamana kwa baadhi ya makosa ya jinai.

Njia nyingine ni kuharakisha usikilizaji wa mashauri, kuwapa uwezo majaji wa Mahakama Kuu kutoa dhamana kwa mashauri ya kesi za udhalilishaji na dawa za kulevya na dhamana hiyo hasa kwa kesi za udhalilishaji kwa watoto wa zaidi ya miaka 15 na kwa chini ya miaka 15 kuendelea kunyimwa dhamana, anasema.

Jaji Ramadhan, anazungumzia malengo na mikakati ya baadaye ya Mahakama Kuu, akitaja kukamilisha ujenzi wa majengo ya kisasa ya mahakama Unguja na Pemba, kuanzisha mifumo ya kisasa ya kielektroniki ya kuendesha shughuli zote za kimahakama ikiwamo kusikiliza na kutoa hukumu kielektroniki au mahakama mtandao.

Aidha, anasema kusimamia na kukuza maadili ya watumishi wa mahakama na mawakili wa kujitegemea, kutumia njia mbadala za utatuzi wa migogoro kama usuluhishi zitatumika ipasavyo ili mashauri yatatuliwe kwa haraka na kukuza imani kwa wananchi kwa mhimili wao wa mahakama.

# Watetezi wa haki wajikumbuka, waanzisha kituo cha kujiganga

**Na Gaudensia Mngumi**

KUNA msemo kuwa mganga hajigangi na kama hivyo ndivyo, wanaharakati watetezi wakuu wa haki za binadamu baada ya kazi ngumu ni nani wa kuwaganga?

Ni baada ya kujiuliza swali hilo, watetezi wa haki za binadamu na za usawa wa kijinsia, wanabaini kuwa kazi hizo zinasababisha maumivu na majeraha moyoni, akili na mwilini hivyo wakati umefika wa kuwa na kituo cha kuwahuisha.

Athari za harakati zinaumiza mwili, moyoni na akili na kusababisha wana harakati kujisahau au kutojithamini, anasema Mary Rusimbi, mwasisi wa kituo cha uponyaji cha Nendiwe Feminist Wellness and Coaching Centre.

Ni kituo cha kutibu majeraha na machungu waliyobaki nayo wanaharakati, akisema wanahitaji uponyaji wa majeraha ya ndani kutokana na viwewe, mihemko, upinzani na changamoto wanazopitia kwenye harakati za kutafuta haki na usawa.

Katika mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam,

wakati wa Tamasha la Jinsia, anapotangaza hoja ya kuanzishwa kituo hicho, anasema ni juhudi zinazofanyika kuyatambua na kubadilisha matokeo ya athari wanaharakati za kifeminia walizopitia wakati wa mchakato wa kufikia haki na usawa wa kijinsia.

"Harakati zinaumiza na wanawake wanahitaji kujifanyia faraja kutokana na kujisahau kwa sababu wana majukumu mengi, mfano ni mama anayetunza familia, ni mwenza kwenye ndoa, kazini na pia ana heshima yake kwenye jamii."

Anasema vyote vinamuhusu kwa kuwa pamoja na kuitwa mama, bibi, mke, mwalimu au profesa chuoni, bado anabaki 'yeye na nafsi yake' na anapotimiza majukumu hayo kila wakati anakutana na maumivu na misuguano.

"Mfano anaumizwa na watoto, mwenza, ofisini pia anapata makovu na majeraha moyoni lakini hata kazi za kiharakati zinamwachia makovu. Hivyo tunahitaji tusitembee na makavu, tupate uponyaji kwa kujitazama," anaeleza Mary.

Akifafanua kuhusu Nendiwe Centre, anasema ni huduma ya kuponywa majeraha kwa vile wengi wanafika kipindi hawajithamini tena na wamechoka.

Anaeleza kuwa wanawake wanaishi na mikwaruzo nyumbani, kazini na hata mitaani lakini kina mama hawauna muda wa kujiangalia na kujiponya nafsi zao ndiyo maana kituo hicho kinaundwa ili kuleta huduma ya pamoja (collective care) ili wasiendelee kutembee na makovu ya harakati.

"Tunachofanya ni kuongeza nguvu ya pamoja kujifundisha ustahimilivu na uhimilivu endelevu kwa kuwa na kituo ili kujifunza na kusaidiana kuondoa makovu rohoni," anasema Mary.

Anaeleza kuwa lengo ni kutibu majeraha na kutembea wakiwa wamepona na kwamba kuna njia nyingi zikiwamo za mbinu za jadi(traditional methods) kama kufurahi michezo, kupaka hina, kufurahiana kwa pamoja.

Uponyaji huo au 'healing justice' unaweza kufanyika kupitia kupambwa kama kupaka hina, kushirikiana kwenye kitchen party, kula na kunywa pamoja na shughuli za kuwaweka pamoja na kupanga mikakati ya kubomoa mifumo kandamizi na kujiinua na kujiwezesha zaidi.

Anagusia kushirikisha visa mkasa, ushuhuda, simulizi, kuwa na mijadala, kukutana kwenye washa na ritiriti na kupata mawazo mapya, uelewa na zaidi kujithamini na kujipa raha baada ya majukumu mengi ya kuchosha ni muhimu.

"Tunataka kujiponya nafsi zetu, tukiibua mbinu za kujipa raha na kujipatia maisha bora zaidi na kujithamini," anasema Mary na kuongeza:

"Tunataka kurudisha tena hali bora kwa wanaharakati ili kujifurahisha, kuongeza nguvu, kuwa wahimilivu zaidi wa changamoto na matatizo na kuwa na afya bora kimwili na kiakili.

## MGANGA HAJIGANGI

Ni muhimu wanaharakati wa haki za binadamu kupata huduma ya 'kuponywa' na athari zilizowaumiza akili, hisia na miili, anasema Roghat Robert, Mkurugenzi wa Shirika la Akili Platform Tanzania.

Akizungumzia umuhimu wa kituo hicho, anaelezea kuwa wanaharakati wanatumia muda, juhudi na kujitoa mno kupigania haki za wanaowatetea na katika harakati hukutana na upinzani kutoka serikalini, kwenye jamii au familia.

Aidha, wanaingia kwenye migogoro na chuki zenye athari kimwili na nafsi na katika hali kama hii hupata onyogovu au kusononeka na majonzi, hivyo ni lazima kupata msaada ili kurudi kwenye ubinadamu.

Robert ambaye shirika lake hujihusisha na afya ya akili, mazingira na haki za binadamu anasema:

"Tunahitaji kujitolea ili kuhudumia watu ili wapate haki zao au kile tunachokitetea hata kama hakuna malipo. Nikumbushe kwenye kutetea haki kuna wanaharakati wanaopoteza, wapo watazamaji na washindi."

Mwasisi wa Akili Platform, anasisitiza kuwa kuwatibu kihisia, akili, nafsi na kimwili ni muhimu kwa vile hawawezi kurejeshewa vile walivyopoteza ikiwamo nguvu na juhudi.

Robert anatoa mfano kuwa mwanaharakati anaweza kula Shilingi 1,000 kati ya 10,000 aliyonayo na kiasi kilichobaki akakitumia kuhudumia anaowatetea akiwapa faraja, kufanya matendo ya huruma, kuwapa nauli kufuata msaada sehemu nyingine na kwamba ndiyo maisha ya wanaotetea haki.

Anasema juhudi hizo huleta onyogovu, akikumbusha kuwa mara nyingi wanaharakati wamesahaulika, kujisahau na kutojithamini na pale anapotokea anayepata tuzo kuna mazingira yaliyomwibua tena wengi hawastahili.

"Wanaofanya harakati hasa hakuna anayewaona, hawafahamiki ila wanaopata tuzo kilichowaibua huenda ni kujuana, nguvu ya pesa hata upendeleo. Ndiyo maana baada ya kujisahau na kusahaulika tunahitaji msaada wa kujikumbuka tena."

Umuhimu wa huduma hiyo haupingwi kwa sababu mwanaharakati anahitaji kupongezwa, kuungwa mkono, kufurahiwa na kushangiliwi na jamii lakini havipati.

Anasema binadamu anaundwa na mambo manne; akili inayolishwa maarifa, roho inayolishwa imani, mwili unaotunzwa na chakula na pia anaundwa na hisia na lazima zote zilishwe.

> Ni muhimu kwa sababu wanaharakati wanachakaa, kuchoka na kituo kitasaidia kupata mawazo mapya na pia hali bora zaidi.

## NJIA ZA UPONYAJI

Anasema wanaharakati wanaponywa kwa semina, kusikiliza masimulizi, kutumia mazungumzo na wazee kuchota hekima na maarifa kwao, mafundisho ya viongozi wa dini akisema ipo nguvu inayoponya inayobebwa na imani.

Anasema kula pamoja ni dawa ya kujiponya, mfano siyo vyakula wala vinywaji ghali ni vile ambavyo kila mmoja angepika kwake, kuvileta na kuviandaa na kula pamoja yote hayo huongeza faraja, uponyaji na kujirudishia upya wa akili na hisia.

"Lakini kujifunza, kusoma, kuandika kazi zetu na mafanikio ili tuendelee kuyafurahia zaidi," anakumbusha.

Mwanaharakati mbobezi Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anaunga mkono kituo cha kuganga wanaharakati, akisema watetezi wa watu wanahitaji kuhuishwa.

Anasema kuanzishwa kituo hicho ni dawa itakayofanikisha kusaidiana, kukuza dhana za kiharakati na kupata ufumbuzi pale wanaharakati wanapopata athari kuanzia za kiakili kiuchumi, afya na hata kukwama.

Anatoa mfano kuwa hata yeye ni mwathirika wa harakati kimwili na kiakili na kuna kipindi aliumia kwenye ajali na alihitaji faraja zaidi, hivyo anaamini kuwa kingekuwapo kingemnusuru.

Anaamini kuwa kuna njia nyingi za kujihuisha za kiasilia au jadi na hata za kisasa, lakini Tanzania eneo hilo lina ombwe ambalo ujio wa Nendiwe Wellness Centre utafungua milango ya kuwa na huduma za kuhuisha mwili, akili na hisia.

"Ni muhimu kwa sababu wanaharakati wanachakaa, kuchoka na kituo kitasaidia kupata mawazo mapya na pia hali bora zaidi. Vitu hivi vipo Afrika Kusini na huenda hiki ni cha kwanza hapa Afrika Mashariki," anasema Dk. Hellen.

Mwanaharakati mwasisi wa harakati za kutetea haki kikiwamo Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Kutoa Msaada wa Kisheria TANLAP.



Mwasisi wa Kituo cha Nendiwe, Mary Rusimbi. **PICHA: WFT-T**

TSHISEKEDI VS KATUMBI

# Uasi wa M23 unavyotishia hatima ya Rais kurejea Ikulu





Wagombea wanaochuana vikali Rais Felix Tshisekedi (kushoto ) na Moise Katumbi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Christina Mwakangale**

Zikiwa zimesalia siku saba 'Wakongomani' kuamua jambo lao, imeripotiwa kuwapo mvutano mkali wa kugombea urais kati ya kiongozi wa sasa wa Congo Felix Tshisekedi na mpinzani wake mkuu Moïse Katumbi.

Wiki iliyopita kuliibuka utata kuhusu uraia wa mgombea Moïse Katumbi, ambao safari hii umeibuka tena.

Tshisekedi, mbali na kampeni za mwishoni mwa wiki, kujinadi kwamba ataboresha hali ya elimu na kuwapo kwa mfumo bure wa elimu, bado mgogoro wa mashariki ya DRC na kundi la M23 kushindwa kupata ufumbuzi unamtia doa.

Katika kampeni zake huko Kivu Kusini, anaahidi kwamba akishinda katika uchaguzi huu, atalisambaratisha kundi la M23.

Zikiwa zimebakia siku saba kabla ya uchaguzi mkuu utakaofanyika Jumatano ijayo Desemba 20, Tshisekedi, anayetetea kiti chake, anaahidi kuimarisha uchumi na kuleta maendeleo kama atachaguliwa tena.

Akiwa mjini Goma, Kivu Kaskazini katika mji wa Beni, kwa ajili ya kampeni hizo za lala salama, licha ya mvua kali, lakini umati wa wafuasi wa chama chake uliingia katika uwanja wa Afya mjini Goma, wakivalia sare nyeupe huku eneo hilo likiwa chini ya ulinzi mkali katika sehemu ambayo mapigano yanaendelea kati ya vikosi vya serikali na waasi wa M23.

Jukwaani anajinadi, akimlaumu jirani yake Rais wa Rwanda Paul Kagame, kwamba ni chanzo cha usalama duni nchini mwake, na kwamba ana mkono kuongeza uasi, akiahidi kurejesha amani na usalama katika eneo hilo.

> Tulipofika madarakani akiba ya nchi ilikuwa dola milioni 840, leo akiba hiyo imefikia dola bilioni tano. Bajeti ilikuwa kwenye dola bilioni tano.

"Hakuna kikubwa kilichosalia ili kumshinda kikamilifu adui. Mniamini. Hivi nitawapa ushindi kamili kwa kulikomboa eneo lote la mashariki mwa Congo," anajinadi Rais Tshisekedi. Unasema mtandao wa TRT Afrika.

Anayataja mafanikio yake kwa wapigakura, akisema kwa miaka mitano yapo mafanikio yanayoshikika.

"Tulipofika madarakani akiba ya nchi ilikuwa dola milioni 840, leo akiba hiyo imefikia dola bilioni tano. Bajeti ilikuwa kwenye dola bilioni tano. Hivi leo tumefikia kwenye dola bilioni16. Ikiwa ntamipa muhula wa pili, nitautumia kuendelea kubuni mipango ya maendeleo," anasema Tshisekedi, kwa mujibu wa TRT Afrika.

Tayari wanafunzi wanasoma bure katika shule za msingi, ikiwa mtanichagua, nitafanya shule ya sekondari kuwa bure na kuimarisha huduma za afya, anasema.

### MPINZANI KATUMBI

Mpinzani mkuu, Moïse Katumbi akiwa jijini Kinshasa mwishoni mwa wiki, anaahidi kuifanya Kinshasa, kuwa mji bora Afrika kwa kuupa miundombinu ya kisasa.

Aidha, Katumbi anaahidi kupunguza gharama za maisha huku akiwataka wafuasi wake wasiondoke kwenye vituo vya kupiga kura kabla ya kuchapishwa matokeo ili kuepuka kile alichokiita, udanganyifu na wizi wa kura uliopangwa.

Uchaguzi mkuu wa Desemba 20 utawahusisha wagombea wa urais takribani 21, lakini mdadisi wa siasa za maziwa makuu Dk.Jumanne Abdoul anasema mchujo umeanza kuonekana, ni katika mazungumzo na DW.

"Baada ya kampeni za wiki tatu, inaonekana wazi kwamba mchuano mkali utakuwa kati ya Tshisekedi na Katumbi. Na inawezekana baadhi ya wagombea wiki hii wakaungana na upande mmoja na mwengine na hapo tunaweza kuanza kuona vizuri sura ya uchaguzi.

Takribani wapigakura milioni 40 wa DRC watamchagua rais katika kinyang'anyiro ambacho Rais Tshisekedi anatafuta muhula wa pili na wa mwisho wa miaka mitano madarakani.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ni taifa kubwa zaidi Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Ikichukua eneo lenye ukubwa wa Ulaya Magharibi yenye idadi ya watu wanaokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 100, nchi hiyo ina utajiri mkubwa wa maliasili kwa mujibu wa DW.

Licha ya baadhi ya wito wa kutaka uchaguzi uahirishwe, mkuu wa tume ya uchaguzi ana imani kuwa kila kitu kitakuwa tayari kwa wakati.

DRC, ina asilimia 70 ya akiba ya dunia ya coltan, madini ya thamani sana ambayo hutumiwa kutengeneza simu za mkononi, pamoja na asilimia 30 ya almasi duniani na kiasi kikubwa cha cobalt, shaba na bauxite.

Makundi ya waasi ni pamoja na M23, Allied Democratic Forces (ADF) na Codeco yanayoendelea kufanya mashambulizi dhidi ya raia na wakilolenga jeshi.

Kutokana na ghasia hizo, DRC ni miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa zaidi ya wakimbizi wa ndani duniani.

Takribani watu milioni 6.9 wanadhaniwa kulazimika kuyahama makazi yao tangu Machi 2022.

Ingawa utajiri wake mkubwa wa madini na idadi kubwa ya watu inawakilisha rasilimali kubwa ya kiuchumi, maisha nchini humo hayajaboreka kwa watu wengi kwa sababu kadhaa, kama vile migogoro, vita vya waasi rushwa na miongo mingi ya utawala mbovu ulioanzishwa tangu nchi hiyo ilipopata uhuru.

Mashariki mwa DRC, sehemu kubwa ya utajiri wa madini, imekumbwa na vita kwa miongo mitatu, vikihusisha waasi wa M23 ambao licha ya jitihada za kuwaondoa vita vya kuwakabili havijaleta amani wala ushindi.

Haijafahamika ni watu wangapi wamepoteza maisha, utafiti wa mwaka 2008 uliofanywa na Kamati ya Kimataifa ya Uokoaji ilikadiria kuwa takribani milioni 5.4 wamekufa, wengi wao kutokana na njaa na magonjwa, na kuifanya idadi hiyo kuwa mbaya zaidi tangu Vita vya Pili vya Dunia. Hata hivyo, tafiti nyingine zimetia shaka juu ya usahihi wa takwimu hizi.

Hata hivyo baada ya miaka mingi ya misukosuko ya kisiasa na mapinduzi ya serikali DRC inaandaa tena uchaguzi tangu kukabidhiwa madaraka kwa amani kati ya Rais wa zamani Joseph Kabila na Tshisekedi mwaka 2019.

### MSURURU WAGOMBEA

Kufuatia kujiondoa kwa wagombea wanne, akiwamo Waziri Mkuu wa zamani Augustin Matata Ponyo, sasa wamebaki 22 wakiwania urais, wakichuana na Tshisekedi.

Wapinzani wake wakuu ni Martin Fayulu, anayeaminika na waangalizi wengi kuwa ndiye mshindi halali wa uchaguzi wa urais wa 2018, ingawa aliibuka wa pili kwa mujibu wa matokeo rasmi.

Moïse Katumbi, mfanyabiashara tajiri na gavana wa zamani wa jimbo la Katanga, na pia mmiliki wa timu ya soka ya TP Mazembe.

Yuko mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel Dk. Denis Mukwege, ambaye alipata ushindi kutokana na kazi yake ya kuwasaidia walionusurika ubakaji.

Wagombea wanne ambao wamejiondoa wote wamemuunga mkono Katumbi na chama chake cha Together for the Republic.

Bado wamo Waziri Mkuu mwingine wa zamani, Adolphe Muzito, mbunge Delly Sesanga, mwanaharakati Floribert Anzuluni na Constant Mutamba. Kinyang'anyiro pia kina wanawake wawili pekee Marie-Josée Ifoku Mputa, mgombea urais mwaka 2018,na Joëlle Bile, anayejinadi kuwa anawakilisha matumaini kwa wanawake na vijana.

### USHINDI WA URAIS

Mgombea atakayepata kura nyingi zaidi katika duru ya kwanza anakuwa rais, akiwa na zaidi ya asilimia 50, kwa hivyo hakuna marudio au duru ya pili.

Vyama vya upinzani vina wasiwasi serikali itafanya udanganyifu katika uchaguzi, vikiishutumu kuzuia uhuru na demokrasia, lakini serikali inakanusha tuhuma hizo.





## Asilimia 43 watoto nchini hawakui kwa utimilifu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

ASILIMIA 43 ya watoto nchini wapo katika hali ya kutofikia hatua timilifu za ukuaji kutokana na viashiria mbalimbali vya hatari ikiwamo utapiamlo, umaskini na kukosekana kwa chakula.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi maalum, Dk. Dorothy Gwajima aliyasema hayo jana alipokuwa akifunga semina ya malezi na makuzi ya watoto jijini hapa.

Alisema hali hiyo inatokana na uwapo wa msongo wa mawazo kwa familia, miundombinu duni na uhaba wa rasilimali kuna changia kwa kiasi kikubwa uwapo wa tatizo la malezi na makuzi kwa watoto.

Dk. Gwajima alisema ili kushughulikia tatizo hilo programu ya malezi na makuzi jumuishi nchini Tanzania zinahitaji kupewa kipaumbele na kuratibiwa vyema ili ziweze kuleta manufaa kwa jamii.

Aidha, Dk. Gwajima alifafanua zaidi ya kuwa utafiti unaonesha kwa kila Dola moja ya Marekani inayowekezwa kwenye afya jumuishi za MMMAM inaweza kuzalisha Dola 17, ushahidi unaonyesha kwamba uwekezaji katika elimu ya awali kwa watoto walio katika mazingira hatarishi unairudisha faida inayokadiriwa kuwa asilimia saba hadi 16 kwa mwaka.

Alisema programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM inalenga kujibu changamoto za mahitaji kwa watoto wadogo ukizingatia ulimwengu mzima una takribani watoto milion 250 wenye umri chini ya miaka mitano ambao wanapatikana kwenye nchi zenye uchumi wa chini.

Alifafanua zaidi ya kuwa program hiyo imefanikiwa kwa haraka na halmashauri 70 zimefanikiwa hadi sasa.

Waziri Gwajima alisisitiza pia halmashauri zote zitenge fedha kwa ajili ya Mpango huo ambao una malengo makubwa ya kufanikisha.

Naye, Mkurugenzi wa Afya,Lishe na Ustawi wa Jamii kutoka TAMISEMI, Dk. Rashid Mfaume alisema ma program hiyo imelenga kuwekeza moja kwa moja kwenye maendeleo ya mwanadamu kwa kukuza malezi jumuishi.

**Waziri Gwajima alisisitiza pia halmashauri zote zitenge fedha kwa ajili ya Mpango huo ambao una malengo makubwa ya kufanikisha.**

# TBS yateketeza bidhaa zisizo na ubora za mamilioni

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeteketeza bidhaa za chakula na vipodozi visivyokuwa na ubora kilo 837,075.07 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 21.8 zilizokamatwa kutoka kwenye maeneo ya biashara kwenye mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora.

Bidhaa hizo zimeteketezwa mwishoni mwa wiki katika dampo la Chidaya jijini hapa baada ya kukamatwa kwenye ukaguzi uliofanyika kwenye maeneo tajwa kati ya Aprili hadi Novemba, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kuteketeza bidhaa hizo, Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS Kanda ya Kati, Vicent Tarimo, alisema bidhaa zilizoteketezwa zinahusisha zilizoisha muda wake wa matumizi, zenye viambata sumu na zile ambazo tarehe ya mwisho wa matumizi zimeharishwa baada ya kuhaririwa.

Kuahirishwa kwa tarehe ya mwisho ya mutumizi ya bidhaa husika kumekuwa kukifanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu. Kwa mujibu wa Tarimo madhara uwepo wa bidhaa zilizoisha muda wa matumizi na zenye viambato sumu ni kuathiri uchumi wa nchi pamoja na afya za watumiaji bidhaa za chakula zilizoisha muda wa matumizi na ambazo tarehe za mwisho wa matumizi zimehaririwa zinaathiri upatikanaji wa virutubisho vinavyotegemewa.

"Bidhaa hizi zinaweza kusababisha magonjwa ya muda mfupi na mrefu ikiwemo saratani," alisema Tarimo.

Kadhalika, alisema katika bidhaa zenye viambata vya sumu athari zake za muda mfupi na mrefu ni pamoja na kuathiri ngozi, macho, mfumo wa uzazi kwa akina mama, ukuaji kwa watoto na magonjwa ya saratani hasa ya ngozi.

"Ukaguzi ni endelevu kwa mikoa yote nchini na wito wangu kwa wafanyabiashara kukagua bidhaa zao mara kwa mara kujiridhisha na ubora wake," alisema.

Aidha, aliwataka kutunza bidhaa hizo kwa mujibu wa taratibu za wazalishaji, kuepuka kuuza bidhaa za vipodozi zenye viambato sumu na kuacha mara moja kuhariri taarifa za mwisho wa matumizi.

Alionya kuwa kali za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa wafanyabishara wasio waaminifu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zake.




Ofisa Operesheni wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma, Deogratius Inano, akionyesha chupa kwa waandishi wa habari juzi, iliyokuwa na mafuta ya taa yanayodaiwa kuwa Rehema Shabani aliyatumia kujimwagia mwilini na kujichoma moto nyumbani kwao Mtaa wa Nduka jijini Dodoma. **PICHA: PAUL MABEJA**

# TRA yakusanya bil. 12.8/- mapato kwa w'biashara

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Singida, imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 12.8 sawa na asilimia 93 ya lengo katika mwaka wa fedha uliopita wa 2022/23.

Meneja wa TRA Mkoa wa Singida, Azaria Kasomi, akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya shukrani kwa mlipa kodi, alisema pamoja na mafanikio hayo kumekuwa na tatizo kwa baadhi ya wafanyabiashara kutotoa risiti kulingana na wanachouza kwa wateja wao.

Kasomi alisema wafanyabiashara lazima watambue kuwa suala la kutumia mashine za EFD na kutoa risiti ni suala ambalo lipo kisheria hivyo hakuna sababu yeyote kwa mfanyabiashara kutozingatia hayo na kujikuta anatozwa faini kitu ambacho TRA haipendi itokee hivyo.

Naye, Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Singida Uchumi na Uzalishaji, Stanslaus Choaji, aliwahimiza wafanyabiashara umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari bila kushurutishwa ili kuchangia pato la taifa na kuiwezesha serikali kuendelea kuboresha huduma mbalimbali za kijamii katika maeneo yao.

"Kodi hizi mnazotoa ndizo zinatumika kupeleka huduma za maendeleo kwa wananchi, mfano katika sekta ya elimu hivyo kunapokuwa na ukwepaji wa kulipa kodi maana yake tunataka kuifanya serikali isipeleke huduma kwa wananchi," alisema.

Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi, Swaumu Mvungi, alisema wafanyabiashara wazingatie sheria zilizopo kulipa kodi kwani kufanya njama za kukwepa kunaleta usumbufu kwa TRA na kusababisha kuchukua hatua.

Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara Wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA), Mkoa wa Singida, Kitila Katala, alisema walipa kodi wanataka kuona kodi wanazotoa zinaleta matokeo chanya katika maendeleo.

Hivi karibuni wakati wa Baraza la Wafanyabiashara, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema serikali imekuwa ikiboresha mazingira ya biashara kwa kuondoa tozo ambazo hazina tija ili kuongeza ukuaji wa biashara na uwekezaji hivyo wafanyabiashara waunge jitihada hizi za Serikali kwa kulipa kodi.

Alisema serikali pia imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa sekta za biashara na uwekezaji zinakuwa na kutoa mchango stahiki katika kukuza uchumi na pato la taifa kwa manufaa ya Watanzania.





# Waomba kuanzishwa h'mashauri mpya Makete

**Na Nebart Msokwa,** MAKETE

WANANCHI wa kata 11 za Bonde la Matamba katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete, mkoani Njombe, wameiomba serikali kuigawa halmashauri hiyo na kuanzisha halmashauri mpya kwa lengo la kuwasogezea huduma na kuchochea shughuli za maendeleo.

Wananchi hao wanapendekeza halmashauri mpya itakayoanzishwa iitwe Halmashauri ya Wilaya ya Kitulo, jina linalotokana na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ambayo inapakana na eneo hilo.

Wakizungumza kwenye kikao cha wadau wa Maendeleo wa Bonde la Matamba, wananchi hao walisema jiografia ya Wilaya ya Makete ni kubwa na yenye milima mingi ambayo inasababisha watumie gharama kubwa kupata huduma za kiutawala kutoka makao makuu ya wilaya yao.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Valentino Malila, mkazi wa Kata ya Matamba, alisema wananchi wanapata shida kufika makao makuu ya wilaya kupata huduma mbalimbali kutokana na jiografia ya wilaya hiyo.

Alisema kuna maeneo ambayo wananchi wanatumia gharama kubwa kusafiri kwenda Makao Makuu ya Wilaya jambo ambalo kutokana na hali ngumu ya uchumi sasa limegeuka kuwa kero kubwa.

"Kwa mfano mwananchi wa Kijiji cha Ikowo akitaka kwenda Makete Mjini, analazimika kuzunguka Makambako kupitia Njombe ndio afike Makete ambako kuna umbali wa zaidi ya kilometa 200 au apitie Mbeya ambako pia kuna umbali wa zaidi ya kilometa 170 hali ambayo inamlazimu kutumia zaidi ya shilingi 80,000 kwenda na kurudi, sasa kutokana na hali ngumu ya uchumi, haya ni maumivu kwa wananchi," alisema Malila.

Alisema hali hiyo inasababisha hata shughuli za kimaendeleo kuzorota kutokana na kukosa hamasa ya viongozi wa kiserikali ambao huchukua muda mrefu bila kuwafikia.

Rhoda Msemwa, alisema ili wananchi wapige hatua kimaendeleo kuna umuhimu mkubwa wa kuanzisha halmashauri mpya katika eneo hilo kwa lengo la kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema halmashauri zipo za ngazi mbalimbali, lakini wao wanachoomba ni halmashauri ya wilaya ambayo wanaamini kuwa wanazo sifa na vigezo vya kusikilizwa ombi lao.

"Tunatambua kuwa zipo halmashauri za ngazi mbalimbali kama vile halmashauri ya kijiji, halmashauri ya mji, manispaa, jiji, lakini sisi tunaomba tupewe halmashauri ya wilaya ambayo tunaamini kuwa tunazo sifa na vigezo vya kuwa halmashauri ya wilaya" alisema Rhoda.

Alisema ikiwa ombi lao litakubaliwa na serikali wanapendekeza jina la Halmashauri mpya itakayoanzishwa iitwe Halmashauri ya Kitulo, kwa heshima ya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ambayo iko kwenye eneo hilo. Akifafanua alisema kuwa jina hilo ni zuri na halitakuwa na mvutano wowote kwa kuwa halina viashiria vya ukabila, dini wala mgongano wowote kwenye jamii yao hivyo litawaunganisha zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alikuwa miongoni mwa waalikwa kwenye kikao hicho na akalazimika kutoa mwongozo ambao wananchi hao wanapaswa kuufuata ili kufikisha ombi hilo serikalini kwa ajili ya utekelezaji.

Alisema Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa sheria, miongozo na maelekezo ya viongozi, hivyo suala hilo lipo kisheria na linapaswa kufuata mchakato wa kisheria kabla ya kutekelezwa.

Makufwe aliwaeleza wananchi hao kuwa ili ombi hilo litambuliwe rasmi ni lazima waanze kufanya mikutano mikuu ya vijiji vyote katika kata hizo 11 na iandikwe mihtasari ambayo itapelekwa kwenye Kamati zao za Maendeleo za Kata (KAMAKA) kwa ajili ya kujadiliwa.

Makufwe alisema kuwa Kamati ya Ushauri ya wilaya nayo ikimaliza kazi yake itawasilisha kwenye Kamati ya Ushauri ya mkoa ambayo pia ikijadili na kuridhia ombi hilo litapelekwa kwa waziri mwenye dhamana ili alifikishe Kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye mwenye uamuzi wa mwisho.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Makete, Clemence Ngajilo, alitoa angalizo kwa wananchi hao akiwataka kujenga umoja na mshikamano ili kufanikisha mchakato wa kuanzishwa kwa wilaya mpya wanayoihitaji.

Alisema ili waweze kufanikiwa ni lazima waendelee kuwa na sauti moja kwenye mapambano ya kupata wilaya mpya wanayoihitaji kwa kuwa anaamini Serikali Kuu na viongozi wake ni wasikivu hasa kwenye suala nyeti kama hilo.



Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wakijadiliana jambo walipotembelea kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari Nyeregete wilayani humo, juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Mary Mbwilo (wa pili kushoto) na kulia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mbarali, Misana Kwangula. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mbaroni tuhuma kutibu mabusha bila vyeti

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia, Abdallah Mohamed Athumani (43), mkazi wa Kijiji cha Mapogolo wilayani Ludewa mkoani Njombe kwa tuhuma za kutoa matibabu ya hospitalini kwa wagonjwa bila ya kuwa na vyeti vinavyomruhusu kufanya shughuli hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe Kamishna Msaidizi, Mahamoud Banga, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, kuwa tukio hilo lilitokea Novemba 30.

Mtuhumiwa huyo alikamatwa akiwa na boksi zaidi ya 23 za vifaa tiba ambavyo vinavyotumika katika hospitali zilizopo hapa nchini.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akiwatibu watu mbalimbali kwa kufanya upasuaji mdogo kama kuondoa mabusha na tezi dume bila ya kuwa na vyeti.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe pia limemkamata Ibrahim Mgimba (25) kwa kushiriki katika kusafirisha vifaa tiba hivyo na kuvificha.

"Kwahiyo hawa wote tutawafikisha mahakamani mara tu upelelezi utakapokuwa umekamilika," alisema Banga.

Wakati huo huo, watu watatu wakazi wa Kibena wilayani Njombe, wanashikiliwa na jeshi la polisi mkoani humo kwa tuhuma za kukutwa na noti bandia za kimarekani dollar 4100 ambazo thamani yake milioni 10.2 za fedha za kitanzania.

Kamanda aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Stanley Menda (23), Priva Lumumba (23) na Asia Kigoda (24).

Tukio hilo lilitokea Desemba 7, Kibena wilayani Njombe.

Alisema katika msako uliofanywa maeneo mbalimbali mkoani humo mwezi Novemba mpaka Desemba jeshi hilo limewakamata watuhumiwa 146 kwa makosa mbalimbali yakiwamo wizi, uvunjaji, uporaji na wizi wa pikipiki.

"Katika operesheni hiyo tumekamata vielelezo mbalimbali ikiwamo dizeli lita 60, simu sita, televisheni saba zikiwamo mbili zilizoibiwa kwenye hospitali ya mkoa wa Njombe," alisema Banga.

# Wanaume wadaiwa kutelekeza watoto wenye ulemavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya wanaume mkoani Mbeya wanadaiwa kuwatelekeza watoto wao wanapobaini kuwa wana ulemavu jambo ambalo linasababisha watoto hao kukosa haki zao za msingi ikiwemo malezi ya wazazi wote wawili.

Wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani humo wamewashauri wanaume wenye tabia za aina hiyo kuacha ili watoto hao wapate malezi sahihi ya wazazi.

Wito huo ulitolewa jana Mkoani Mbeya,na wadau wa kupinga ukatili wa kijinsia walipotembea,ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia.

Mkurugenzi wa kituo cha kuhudumia watoto wenye ulemavu cha Shirika la Watumishi wa Upendo cha Kanisa Katoliki Parokia ya Iwindi, Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya, Padri Herman Mongi, alitoa ushauri huo juzi alipozungumza na baadhi ya wadau walitembelea kituo hicho kwa lengo la kuwafariji watoto hao.

Alisema idadi kubwa ya watoto wenye ulemavu waliopo kituoni hapo wametelekezwa na baba zao na kuwaachia mzigo wa malezi akina mama ambao pia hawamudu mahitaji yao hali inayowapa wakati mgumu wa malezi.

"Kituo chetu kina watoto 207 ambao wengi yu wachanga na wengi wao wameletwa na kinamama ambao wametelekezwa na waume zao kwa hiyo inatupa changamoto ya kuhudumia mama na mtoto kwa sababu kama mama hana chakula hatuwezi kumuacha na njaa," alisema Padri Mongi.

Alisema kwa sasa uelewa kuhusu kuwaficha watoto wenye ulemavu umeongezeka kutoka na wazazi kuwapeleka kwenye vituo vya kuhudumia walemavu pale wanaposhindwa kuwahudumia na hivyo akasisitiza elimu kuendelea kutolewa kwa jamii ili watoto hao wapate haki zao.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali, alisema kama wadau wa kupinga ukatili wamekutana na shuhuda za watoto wenye ulemavu waliopata ujauzito katika umri mdogo liche ya ulemavu wao.

Aliwataka wanaume wanaowapa ujauzito watoto wenye ulemavu kuacha tabia hiyo.

Tabitha aliwataka wanaume kushirikiana na wake zao katika malezi ya Watoto hao ili wapate mahitaji yao muhimu ikiwamo kuwapeleka shule kwa kuwa sera za serikali zimeweka elimu jumuishi kwa watoto wote.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Lilian Kilongumtwa, alisema mtoto mwenye ulemavu sio laana kwenye familia kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakifikiria.

Alisema kuwafungia ndani ni kuwakatili hivyo akawataka wazazi na walezi kuwapatia mahitaji yote wanayohitaji na kwamba serikali itaendelea kushirikiana kutoa vifaa saidizi kwa walemavu na kuhakikisha wanapata haki zao zote za msingi ikiwemo elimu.



## Viongozi watakiwa kujaza fomu za maadili kabla 2024

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema viongozi wanapaswa kujaza fomu za maadili hivi sasa kwa kupitia mfumo wa njia ya kielektroniki.

Suleiman alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, wakati akiwasilisha ripoti ya saba ya utekelezaji wa kazi za Tume ya Maadili kwa mwaka 2022-2023 mbele ya wajumbe wa baraza hilo.

Alisema ili kuendana na maendeleo ya mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Tume imeandaa fomu kwa viongozi kujaza moja kwa moja kupitia njia hiyo ambayo ndiyo inayokubalika katika mageuzi ya sasa.

Alisema viongozi ambao taasisi zao zimeunganishwa na mkongo wa taifa, ndiyo watakaoanza kupata huduma za fomu hizo kujaza kwa njia ya mtandao.

Alisema hatua ya kujaza fomu za maadili kwa njia ya kielektroniki kutaongeza ufanisi na kutoa fursa kwa viongozi kuingiza taarifa zao za mali na mapato na madeni wanapopata mabadiliko kuliko kusubiri kipindi cha mwisho wa mwaka.

Malalamiko yanayohusiana na uvunjwaji wa maadili, waziri alibainisha kuwa Tume imepokea 19 na kufanyiwa kazi ikiwa ni sawa na asilimia 95 ya shabaha iliyokadiriwa.

Alisema miongoni mwa malalamiko hayo yanahusishwa na watendaji wa wizara, idara na taasisi za serikali ya mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema viongozi wengi wanakabiliwa na tuhuma za matumizi mabaya ya nafasi ikiwamo rushwa na mgongano wa maslahi na matumizi mabaya ya teknolojia ya mawasiliano.

# Shirika la Nyumba Z'bar kupunguza umaskini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba Zanzibar, Mwanaisha Ali Said, amesema lengo la shirika ni kuchangia ukuaji wa uchumi ili kupunguza umaskini kupitia maendeleo ya miundombinu ya makazi na uwekezaji pamoja na utoaji wa huduma za uhandisi na ujenzi.

Akitoa maelezo ya historia ya Shirika hilo kwa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Nyumba la Taifa Tanzania (NHC), kabla ya kufanya ziara kwenye maeneo ya miradi ya ujenzi, alisema azma ya shirika hilo ni kujenga nyumba kupitia miradi mbalimbali ili kujikwamua kiuchumi na kuwapatia makazi bora wananchi yenye gharama nafuu. Aidha, alisema kwa msaada wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Husein Ali Mwinyi, wameendeleza mradi mpya wa nyumba za Mombasa Kwamchina ambazo hadi sasa asilimia 80 ya nyumba hizo zimeshauzwa.

Alisema mkakati uliopo kwa sasa ni kuyapunguza majengo mabovu ya mji mkongwe kwa kuwapa wawekezaji kuyafanyia ukarabati ili yasijeleta athari kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

"Kutokana na matengenezo ya majengo hayo yanachukuwa muda mrefu na gharama zake ni kubwa hivyo tuliona iko haja kuwapatia wawekezaji," alisema Mwanaisha.

Alisema hiyo imetokana na majengo hayo kuwa na gharama kubwa na makusanyo yanayokusanywa ni madogo pamoja na hayo wapangaji hawalipi kodi ipasavyo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdalla, alisema wamesaini mkataba wa ushirikiano na Zanzibar mwezi Agosti, mwaka huu na wakifanya kazi zao kwa karibu kuhusu masuala ya teknolojia katika pande zote mbili pamoja na kubadilishana wafanyakazi ili kujifunza na kubadilishana uzoefu.

Alisema walifika Zanzibar wakijumuika na wakurugenzi wa bodi ambao ndio wanaofanya maamuzi yote ya Shirika kwa mwendelezo wa ushirikiano pamoja na kujifunza mambo mbalimbali.

"Miongoni mwa mambo waliyojifunza ni sera ya Zanzibar ambayo ukinunua nyumba kutoka (Zanzibar House Cooperation) hulipi kodi la ongezeko la thamani ukija bara zile nyumba zenye thamani ya milioni 50 kuanzia mwezi Julai ndizo ambazo hazilipiwi kodi, jambo ambalo linaongeza gharama ni kodi," alisema.

Aidha, alisema Zanzibar wamesharuhusu diaspora kununua nyumba na wageni ambao sio raia wa Tanzania kununua pamoja na kuanzisha miradi ya ujenzi wa nyumba.

Ziara hiyo ni ya siku moja walitembelea miradi ya ujenzi ikiwamo wa nyumba darajani, maduka ya biashara Mkunazini, nyumba za maendeleo Michenzani, Nyumba za makazi na biashara Mombasa pamoja na eneo la ujenzi wa nyumba mpya za kisasa.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba (ZHC) Zanzibar, Mwanaisha Ali Said, akiwasilisha mada katika kikao cha kujenga uzoefu katika shirika hilo na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), mjini Unguja jana. **PICHA: MAELEZO**

# Wanafunzi waandaliwa mikakati mizuri kufaulu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inaendelea kuchukua jitihada za kuaanda mazingira bora ya kujifunza kwa wanafunzi ili kufanya vizuri katika mitihani yao ya taifa.

Hayo yalisemwa visiwani humo jana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohammed Mussa, wakati akizindua ripoti ya utafiti wa afya na lishe pamoja na mkakati na mwongozo wa elimu ya afya na lishe kwa wanafunzi.

Alisema katika kufanikisha uwezo mzuri wa kusoma na kuandika wanafunzi chini ya miaka mitano hadi 19 imebainika kuwa lishe zao zimeonekana kuwa na uhaba wa kula vyakula vyenye lishe.

Alisema katika utafiti uliyofanywa mwaka 2022 matokeo yameonesha kuwa upande wa ulaji wa vyakula unaofaa makundi sita ya vyakula ni asilimia 48.0 wanatumia samaki, asilimia 69.8 wanatumia mboga na matunda yenye vitamin A na asilimia 56.7 wanatumia mboga za kijani kibichi angalau mara nne kwa wiki.

Alisema ukosefu wa lishe ni changamoto kwa nchi zinazoendelea hivi sasa kutokana na changamoto mbali mbali hasa za kimaisha.

Aidha, alisema kwa mujibu wa Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya watoto milioni 17 duniani wameathirika na utapia mlo uliokithiri.

Waziri Lela alisema kwa Zanzibar utafiti wa afya na lishe katika shule uliofanyika mwaka 2022 kwa watoto na vijana wenye umri kati ya mikaka mitano hadi 19, matokeo yanaonesha kuwa kiwango cha udumavu ni asilimia 15.6.

"Kutokana na utafiti huo hii inaonyesha kuwa takribani watoto wawili katika kila watoto 10 urefu wao hauna ulingano na umri wao, na kiwango cha uzito pungufu ni asilimia 13.3 uzito kupitiliza au unene uliyokithiri ni asilimia 8.4 na upungufu wa damu umeripotiwa kuwa asilimia 45.7," alisema.

Alisema matokeo ya utafiti huo yameonesha kuwa miongoni kwa sababu zinazochangia matatizo ya lishe Zanzibar kwa watoto na vijana ni pamoja na ulaji wa vyakula usiridhisha.

Alisema karibu ya robo ya watoto na vijana asilimia 26 walihojiwa, katika mazingira ya shule hutumia vinywaji vyenye sukari kama juisi na ice cream ambavyo vyakula hivyo vinasukari nyingi na hatari kwa afya ya binadamu.

Alisema kwa upande mwengine asilimia 50.4 ya watoto na vijana wenye umri wa balehe hushindwa kuwa mahiri katika kufuatilia masomo yao au katika shughuli zao wakati wa asubuhi kutokana na kukosa kifungua kinywa.

Alisema bado mazingira ya shule yamekuwa kikwazo katika kuhamasisha ulaji bora na utafiti huo umebaini kuwa asilimia 79 ya maduka na wauzaji wanaozunguka mazingira ya shule wanauza vyakula visivyo na ubora.

Alisema ili kupambana na hali ya lishe Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imeandaa mwongozo na mikakati maalum wa elimu ya afya na lishe ambao utatumika katika shule za Zanzibar.

Naye Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Salum Kassim Ali, alisema uzinduzi huo wa utafiti uliofanyika mwaka 2022 umetokana na changamoto mbalimbali kwa watoto wa miaka mitano hadi 19.

Alisema utafiti huo uliwashirikisha wanafunzi katika shule kwa kufanyiwa mahojiano, wanafunzi 1,322 walikuwa wanawake na 1,234 wanaume kwa lengo la kubaini changamoto katika masuala ya lishe.

Mwakilishi mkaazi kutoka Global Affair Canada Tanzania, Eike Wisch, alisema taasisi yake iko mstari wa mbele katika kushirikiriana na Serikali ya Zanzibar suala la afya kwa watoto.

Alisema kuwa Serikali ya Zanzibar imepiga hatua za maendeleo katika kuwajali watoto na vijana hasa katika mipango yake ya maendeleo ya afya kwa wote.

Mwakilishi mkaazi kutoka UNICEF Tanzania, Hele Fiche alisema katika kufikia maendeleo endelevu ya watoto na vijana kuna kila sababu ya kupatiwa lishe kwa ajili ya makuzi yao.

Alisema serikali ina mwamko wa kuwapatia afya bora watoto na vijana ili kutengeza taifa bora la baadae na kuwajengea afya bora.

# WHO yasisitiza ulinzi wa kibinadamu kwa wagonjwa

## • Ni baada ya hali kuzidi kuwa tete Gaza



Majeruhi wa Kipalestina wakiwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa huduma ya matibabu huko Ukanda wa Gaza. **PICHA: MTANDAO**

**JERUSALEM,** Israel

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limetoa wito wa kusisitiza Israel na Hamas kuhakikisha ulinzi wa huduma za afya na usaidizi wa kibinadamu huko Gaza wakati wa utekelezaji wa zoezi la kuhamisha wagonjwa mahututi kutoka hospitali za Gaza Kaskazini kwenda Kusini.

WHO inatoa wito huo jana baada ya ucheleweshaji unaotajwa kujitokeza katika vituo vya ukaguzi vya kijeshi jambo linalotajwa kusababisha mgonjwa kufariki, sambamba na kuzuiliwa kwa washirika wa afya wakati wa misheni ya kuhamisha wagonjwa mahututi na kupeleka vifaa katika hospitali kaskazini mwa Gaza.

WHO inasema kwa kushirikiana na Shirika la Msalaba Mwekundu la Palestina (PRCS), Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Masuala ya Kibinadamu (OCHA), na Idara ya Usalama ya Umoja wa Mataifa (UNDSS), ilikamilisha misheni ya kupeleka vifaa vya matibabu katika Hospitali ya Al-Ahli, na kuhamisha wagonjwa waliojeruhiwa vibaya.

Inaelezwa kuwa ujumbe huo ulipeleka vifaa ikiwamo vya upasuaji vilivyotosha kuwatibu wagonjwa 1500, na kuwahamisha wagonjwa mahututi 19 pamoja na masahaba 14 hadi 'Nasser Medical Complex' kusini mwa Gaza, ambako wanaweza kupata huduma kubwa ya matibabu.

WHO inabainisha kuwa wakiwa njiani kuelekea kaskazini, msafara wa UN ulikaguliwa katika kituo cha ukaguzi cha Wadi Gaza, na wafanyakazi wa ambulensi walilazimika kuyaacha magari hayo ili kutambulishwa.

### VITISHO

Aidha, inaeleza kuwa wafanyakazi wawili wa PRCS walizuiliwa kwa zaidi ya saa moja na kuchelewesha misheni, na kwamba wafanyakazi wa WHO waliona mmoja wao akipigwa magoti kwa kunyooshewa bunduki na kisha kuondolewa asionekane kwamba alinyanyaswa, kupigwa, kuvuliwa nguo na kupekuliwa.

Inabainishwa kuwa wakati ujumbe huo ukiingia katika mji wa Gaza, lori la msaada lililokuwa limebeba vifaa vya matibabu na moja ya ambulensi ilipigwa na risasi.

Inaelezwa kuwa wakiwa njiani wakirudi kuelekea kusini mwa Gaza, wakiwa na wagonjwa wa Hospitali ya Al-Ahli, msafara huo ulisimamishwa tena katika kituo cha ukaguzi cha Wadi Gaza, ambako wafanyakazi wa PRCS na wagonjwa wengi walilazimika kuacha ambulensi kwa ukaguzi wa usalama.

Wagonjwa mahututi waliosalia kwenye magari ya kubebea wagonjwa walipekuliwa na askari wenye silaha. Na kwamba mmoja ya wafanyakazi hao wawili wa PRCS waliozuiliwa kwa muda mapema wakiwa njiani na kuchukuliwa kwa mahojiano kwa mara ya pili.

> Inakabiliwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa kiwewe ndani ya hospitali, na nje ya barabara, madaktari wanalazimika kutanguliza ni nani anayepokea huduma na nani asiyepokea huduma.

WHO inasema ujumbe huo ulifanya majaribio mengi ya kuratibu kuachiliwa kwake, lakini baada ya zaidi ya saa mbili na nusu iliwabidi kufanya uamuzi mgumu wa kuondoka eneo hilo hatari na kuendelea, kwa usalama na ustawi wa wagonjwa na wafanyakazi wa kibinadamu.

PRCS iliripoti kwamba wakati wa mchakato wa uhamisho, mmoja wa wagonjwa waliojeruhiwa alikufa, kutokana na majeraha yake ambayo hayajatibiwa. Huku ikibainisha kuwa mfanyakazi wake aliyekamatwa aliachiliwa baada ya kiza kuingia.

Inasema jana ujumbe huo ulikutana naye akiwa na wafanyakazi wenzake, akieleza kuwa alinyanyaswa, kupigwa, kutishiwa, kuvuliwa nguo na kufungwa macho, mikono yake ilikuwa imefungwa nyuma ya mgongo wake na alitendewa udhalilishaji.

Hata hivyo inaelezwa kuwa watu wanne kutoka Wizara ya Afya na mfanyakazi mmoja wa PRCS bado wako kizuizini, na kwamba zaidi ya wiki tatu sasa hakuna habari juu ya ustawi wao au mahali walipo, ikisisitiza kwamba suala hilo halikubaliki.

"WHO pamoja na familia zao, wafanyakazi wenzao na wapendwa wao, wanahangaikia sana hali njema yao. Tunakariri wito wetu wa kutaka haki zao za kisheria na za kibinadamu ziheshimiwe. Kuzuia ambulensi na mashambulizi dhidi ya wahudumu wa kibinadamu na wa afya ni jambo lisilofaam," imesema WHO.

"Huduma za afya, ikiwa ni pamoja na ambulensi, zinalindwa chini ya sheria za kimataifa. Lazima ziheshimiwe na kulindwa katika hali zote. Matatizo yanayokabili ujumbe huu yanaonyesha kupungua kwa nafasi kwa wahusika wa misaada ya kibinadamu kutoa misaada ndani ya Gaza," imesema WHO.

"Ingawa ufikiaji unahitajika sana ili kupunguza hali mbaya ya kibinadamu, kama inavyotakiwa katika azimio lililopitishwa na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya WHO Desemba 10," imesema.

### MSIMAMO WA WHO

WHO na washirika wanasalia na nia thabiti ya kukaa Gaza na kusaidia idadi ya watu. Lakini kadiri uhasama unavyoongezeka kote Gaza, misaada inapungukiwa na mahitaji, mfumo wa usaidizi wa kibinadamu unakaribia kusambaratika.

Inasisitiza kwamba suluhisho pekee inalowezekana ni usitishaji vita endelevu, na kwamba WHO na washirika wake wanaweza kufanya kazi kwa usalama na bila vikwazo ili kuimarisha mfumo wa afya unaozorota, kujaza vifaa muhimu vya mafuta, dawa, na misaada mingine muhimu, na kuzuia magonjwa, njaa, na mateso zaidi katika Ukanda wa Gaza.

### HALI ILIYOPO

Vile vile inaeleza kuwa wakati wa misheni ya kuwahamisha wagonjwa katika mji wa Gaza ulioharibiwa, wafanyakazi wa WHO waliona mamia ya watu, ikiwa ni pamoja na wanawake, wazee, vijana na watoto, ambao walionekana kushangaa kuona wafanyakazi wa misaada katika eneo hilo kutokana na ukosefu wa usalama.

Wafanyakazi wa WHO walielezea Hospitali ya Al-Ahli kuwa katika hali ya machafuko makubwa na eneo la maafa ya kibinadamu. Na kwamba ina msongamano mkubwa wa watu wengi waliokimbia makazi yao na zaidi ya wagonjwa 200, wakati ina rasilimali za kutosha kuhimili vitanda 40 ikiwa ni nusu ya uwezo wake wa awali wa vitanda.

Madaktari wanasema hali hiyo imeshindwa kudhibitiwa kwani wanakabiliwa na uhaba wa mafuta, oksijeni, na vifaa muhimu vya matibabu, pamoja na ukosefu wa chakula na maji kwa wagonjwa na wao wenyewe.

Inaelezwa kuwa uwezo wa wafanyakazi wa afya ni mdogo sambamba na huduma ya uuguzi usiojitosheleza, huku hospitali ikitegemea watu wanaojitolea.

"Inakabiliwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa kiwewe ndani ya hospitali, na nje ya barabara, madaktari wanalazimika kutanguliza ni nani anayepokea huduma na nani asiyepokea huduma," imesema WHO.

"Wanatibu kesi nyingi mbaya katika korido za hospitali, sakafuni, katika kanisa la hospitali, na hata mitaani. Hospitali hiyo ina wahudumu wa muda mfupi sana, na haina uwezo wa kufanya upasuaji wa mishipa. Kukatwa kwa viungo huamuliwa kama njia ya mwisho kuokoa maisha," imesema WHO.

# KOCHA AZAM AKUNWA KASI YAO USHINDI LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry, amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kujitoa katika michezo yao na kufanikiwa kuvuna alama tatu katika michezo mitatu mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo wa Azam FC, aliyaongea hayo juzi baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mchezo wa ligi hiyo dhidi ya JKT Tanzania na kuibuka na ushindi wa mabao 2-1, katika Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

**Ferry alisema amefurahi kuona mechi ya tatu timu yake ikiendelea kupata pointi tatu katika timu ngumu na zenye ushindani mkubwa ikiwamo dhidi ya JKT Tanzania juzi.**

"Haikuwa mechi rahisi sana kama nilivyosema awali kuwa tunaenda kukutana na timu nzuri na yenye ushindani mkubwa, nawapongeza wachezaji wetu wanavyopambana na kufanikiwa kuvuna alama tatu muhimu dhidi ya JKT Tanzania.

"Kipindi cha kwanza kilikuwa kigumu kwa wapinzani kucheza vizuri na tulipoenda mapumziko tukawaeleza wachezaji nini cha kufanya, hivyo tukafanikiwa kupata ushindi na alama tatu muhimu," alisema Ferry.

Naye Kocha Msaidizi wa JKT Tanzania, George Mketo, alisema walicheza mpira mzuri na wachezaji walifuata maelekezo yao, lakini walifanya makosa ambayo yamewagharimu.

"Niwapongeze Azam FC kwa kufanikiwa kupata matokeo mazuri kwa kutumia makosa tuliyofanya hivyo kuibuka na alama tatu, nawapongeza pia wachezaji wangu kwa kufuata maelekezo na kucheza katika mipango yetu," alisema Mketo.

# New Generation Queens yapania kutetea ubingwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kuanza vema Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar kwa kutoa kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Island Queens, Kocha Mkuu wa New Generation Queens, Ahmad Ali Bakari, amesema mipango yake ni kuhakikisha anatetea ubingwa wao msimu huu.

New Generation Queens, ambao ni mabingwa watetezi wa ligi hiyo, katika mchezo huo uliopigwa juzi kwenye Uwanja wa Mau B, majira ya saa 10 alasiri, mabao yao yalifungwa na Hawa Ally dakika ya 35 na Haida Aidar aliyepachika bao la pili dakika ya 78 huku lile la kufutia machozi kwa upande wa Island Queens likifungwa na Zalia Salum dakika ya 60.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Mkuu wa New Generation Queens, Bakari alisema kushinda mchezo wao huo wa kwanza umewapa nguvu na mwanga wa kufanya vizuri katika michezo yao ijayo.

Alisema ni kawaida ligi inapoanza kuwa ngumu kwa kuwa kila timu inahitaji kufanya vizuri ili kupata alama zitakazomfanya kuwa juu katika msimamo wa ligi, hivyo na wao wamejiandaa kukabiliana na hali hiyo.

"Ligi yetu ni ngumu kwa sababu timu zote wachezaji wao wanajuana na viwango vipo sawa, hivyo tunahitaji kucheza kwa tahadhari zaidi ili kuhakikisha hatupotezi malengo yetu mapema," alisema.

Akiuzungumzia mchezo wao huo, alisema licha ya kutoka na ushindi, lakini timu yake haikucheza vizuri kama ilivyozoeleka.

Alisema bado timu yake haijaungana vizuri kati ya wachezaji wa zamani na wachezaji wapya ambao wamesajiliwa msimu huu.

Hata hivyo, kocha huyo amewataka mashabiki wa timu hiyo yenye makazi yake Kwahani, kujitokeza kwa wingi uwanjani kila inaposhuka dimbani ili kuwapa wachezaji sapoti na ari ya upambanaji.

## ZAIDI YA KIPAJI...



Mtoto, Aikom Aljanat, akipiga mpira kurudisha kwa mpinzani wake hayupo pichani, wakati wakifanya mazoezi ya mchezo wa Tenis katika viwanja vya Gmykhana jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ATCL kumsafirisha bure miss Tanzania

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Ndege (ATCL), imeingia makubaliano na Kampuni ya The Look Company Limited, kumwezesha Miss Tanzania 2022, Halima Kopwe, kushiriki mashindano ya kumsaka Mrembo wa Dunia maarufu "Miss World" yanayotarajiwa kufanyika Machi mwakani, nchini India.

Makubaliano hayo yalisainiwa jana kwenye Ofisi za ATCL jijini Dar es Salaam baina ya Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi na Mkurugenzi wa The Look Company, Basilla Mwanukuzi.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo, Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Matindi alisema Air Tanzania imekuwa mdau mkubwa katika kuunga mkono sekta ya utamaduni, sanaa na michezo kwa ajili ya kukuza vipaji vya vijana wa Kitanzania na kuimarisha tasnia hiyo muhimu kwa maendeleo ya nchi.

"Ni kwa muktadha huo leo kwa furaha tunatangaza rasmi makubaliano yetu na kampuni inayoratibu mashindano ya warembo nchini, The Look Company Limited, kumwezesha Miss Tanzania 2022, Halima Kopwe, kushiriki mashindano ya kumsaka Mrembo wa Dunia maarufu kama Miss World yanayotarajiwa kufanyika Machi 2024, nchini India," alisema.

Alisema Air Tanzania itampatia Miss World Tanzania, Halima Kopwe, ufadhili wa tiketi ya ndege ya daraja la hadhi ya juu kabisa la ndege za shirika hilo (Daraja la Biashara) kutoka Dar es Salaam, Tanzania hadi Mumbai, India.

Matindi alisema wateja wa Air Tanzania wanaotumia Daraja la Biashara hupata huduma za ziada ili kuwawezesha abiria kusafiri kwa raha na starehe kwa kuzingatia mahitaji ya wateja yanayobadilika na ushindani wa soko.

"Ni imani yetu kuwa, kwa heshima hii Air Tanzania tuliyompa Halima Kopwe kutumia daraja la biashara hadi Mumbai nchini India, kutamuongezea hamasa na ujasiri zaidi na kuhamasisha vijana wengi nchini kuendelea kupigania ndoto zao," alisema.

Halima alisema mashindano hayo yatafanyika kuanzia mwezi wa pili na wa tatu mwakani na kwamba yeye atakaa kambini kwa maandalizi kwa muda wa mwezi mmoja.

Mkurugenzi wa The Look Company, Basilla Mwanukuzi, alisema ubia huo na Kampuni ya Ndege ya ATCL utamwezesha mrembo huyo kusafiri na ndege za serikali bure jambo ambalo alisema litampa heshima kubwa.

"Halima atakwenda kwenye mashindano hayo kwa heshima zote akiwa amepelekwa na ndege ya serikali, fainali ni mwezi wa tatu, lakini Halima ataenda mwezi wa pili kwa ajili ya kambi ya mwezi mmoja," alisema.

## ZISIKUPITE

### GALLAGHER KUUZWA

CHELSEA iko tayari kupokea maombi ya kumuuza kiungo wa England, Conor Gallagher, 23, wakati dirisha la uhamisho litakapofunguliwa mwezi ujao ili kumtafutia fedha kocha Mauricio Pochettino, ambaye anaweza kumnunua mshambuliaji wa Brentford na England, Ivan Toney, 27, au mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen. ***(Mail)***

### DISASI, CUCURELLA NAO

MLINZI wa Ufaransa, Axel Disasi na beki wa Hispania, Marc Cucurella ni miongoni mwa wachezaji saba ambao Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino yuko tayari kuwauza Januari. ***(Teamtalk)***

### SANCHO, RAPHINHA KUPISHANA

KLABU ya Manchester United inataka kubadilishana winga wa England, Jadon Sancho, 23 na winga wa Barcelona na Brazil, Raphinha, 26. ***(Sport)***

### MARTIAL, UNITED KUACHANA

MANCHESTER United haina nia ya kutumia chaguo la kuongeza muda mkataba wa mshambuliaji wa Ufaransa, Anthony Martial, 28, utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Athletic)***

### CASEMIRO KUWEKWA SOKONI

KLABU ya Manchester United iko tayari kupokea maombi ya kuwauza kiungo wa kimataifa wa Brazil, Casemiro, 31, mlinzi wa zamani wa Ufaransa, Raphael Varane (30) na kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek (26), Januari, pamoja na Martial na Sancho. ***(Guardian)***

### DIALLO KIKOSI CHA KWANZA

IWAPO Jodan Sancho ataondoka Manchester United, mshambuliaji wa Ivory Coast, Amad Diallo, 21, anaweza kuchukua nafasi yake katika kikosi chao cha kwanza baada ya kuuguza jeraha lake. ***(Football Insider)***

### WEST HAM NA MOYES

KLABU ya West Ham United inabakia kwa asilimia 100 nyuma ya David Moyes, 60, licha ya kufungwa mabao 5-0 ugenini na Fulham. ***(Telegraph)***

### PALHINHA AWANIWA BAYERN

WAWAKILISHI wa Bayern Munich walikuwa kwenye mchezo wa Jumapili kumfuatilia kiungo wa kati wa Fulham na Ureno, Joao Palhinha, 28, ambaye nusura wamsajili msimu uliopita. ***(90min)***

### UDOGIE MKATABA MREFU

KLABU ya Tottenham Hotspur imekubali mkataba mpya wa muda mrefu kwa beki wa Italia, Destiny Udogie, 21. ***(Fabrizio Romano)***


### HOLGATE KUREJESHWA

KLABU ya Everton inataka kumrejesha mlinzi wa England, Mason Holgate, 27, kutoka kwa mkopo wake wa muda kule Southampton kwa sababu hapati muda wa kucheza. ***(Sun)***

### KELLY KITITA KIKUBWA

KLABU ya Bournemouth imempa Lloyd Kelly, 25, mkataba wa kitita kikubwa kwenye klabu hiyo katika jitihada za kumshawishi kutia saini mkataba mpya. ***(Teamtalk)***

## DONDOO SOKA
## MAGAZETI ULAYA




# OSIMHEN NA DADA YAKE WANASOKA BORA AFRIKA

**MARRAKECH,** Morocco

**●●● Watunukiwa tuzo hiyo huku Percy Tau akiibuka mchezaji bora wa...**

MSHAMBULIAJI wa Nigeria, Victor Osimhen, ametawazwa kuwa Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Afrika baada ya kumshinda Mohamed Salah kwenye tuzo zilizofanyika jijini Marrakech nchini Morocco Jumatatu usiku, huku Asisat Oshoala ambaye ni 'dada yake' kutokana na kutoka nchi moja' akishinda kwa upande wa wanawake.

**Osimhen mwenye umri wa miaka 24, alifunga mabao 26 alipoisaidia Napoli kutwaa ushindi wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu uliopita ikiwa ni mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 33.**

Mshambuliaji wa Liverpool na Misri, Salah na beki wa kulia wa Paris Saint-Germain na Morocco, Achraf Hakimi walikuwa wachezaji wengine wawili walioingia kwenye fainali, lakini Osimhen alishinda tuzo hiyo na kuwa mshindi wa kwanza kutoka Nigeria tangu Nwankwo Kanu mwaka 1999.

"Ni ndoto iliyotimia. Lazima nimshukuru kila mtu ambaye amenisaidia katika safari hii na Waafrika wote ambao wamesaidia kuniweka kwenye ramani licha ya makosa yangu," alisema Osimhen.

Morocco ilishinda tuzo ya Timu ya Taifa ya Mwaka baada ya kufika nusu fainali ya Kombe la Dunia nchini Qatar mwaka jana, huku kocha wao, Walid Regragui akishinda Kocha Bora wa Mwaka.

Mshambuliaji wa Timu ya Wanawake ya Barcelona na raia wa Nigeria, Oshoala alitwaa tuzo ya Mwanasoka Bora wa Afrika kwa Wanawake ikiwa ni kwa mara ya sita.

Kocha Bora wa Mwaka (wanawake): Desiree Ellis (Afrika Kusini) Timu ya bora ya taifa ya mwaka (wanaume): Morocco

Timu ya bora ya taifa ya mwaka (wanawake): Nigeria

Kipa bora wa mwaka (wanaume): Yassine Bounou (Al Hilal & Morocco)

Kipa bora wa mwaka (wanawake): Chiamaka Nnadozie (Paris FC & Nigeria)

Mchezaji bora chipukizi wa mwaka (wanawake): Nesryne El Chad (Lille & Morocco)

Mchezaji bora chipukizi wa mwaka (wanaume): Lamine Camara (Metz & Senegal)

Klabu bora ya mwaka (wanawake): Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini)

Klabu bora ya mwaka (wanaume): Al Ahly (Misri)

Mchezaji bora wa mwaka wa Klabu barani Afrika (Wanaume): Percy Tau (Al Ahly & Afrika Kusini)

HABARI MICHEZO



# RAIS BARCA SASA ANOGEWA NA JOAN FELIX

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta amepanga kukutana na kufanya mazungumzo na wawakilishi wa mshambuliaji wa Atletico Madrid anayecheza kwa mkopo kwenye kikosi chao, Joao Felix na kiungo, Joao Cancelo ambaye anacheza kwa mkopo akitokea Manchester City.

Mastaa hao ambao wote wanatokea Ureno wameonesha viwango vya kuvutia na Barca imepanga kuwasajili jumla ama kuwachukua tena kwa mkopo kuelekea msimu ujao.

Taarifa za awali zinaeleza Atletico Madrid inahitaji kiasi kisichopungua pauni milioni 60 hadi 68 ili kumuuza Felix wakati Man City ikihitaji pauni milioni 44 kumwachia Cancelo.

Hata hivyo, mabosi wa Barca wanaona fedha hizo ni nyingi hivyo wamepanga kuzishawishi pande zote kuhakikisha wanapunguza bei ili waweze kukamilisha dili hizo katika dirisha lijalo la usajili au mwishoni mwa msimu.

Tangu atue Barca, Felix mwenye umri wa miaka 24, ambaye mkataba wake na Atletico unamalizika mwaka 2029, amefunga mabao matano kwenye mechi 17 za michuano yote alizocheza wakati Cancelo mwenye umri wa miaka 29, akifunga mabao matatu katika mechi 17.

# *McTominay: Wachezaji tunasimama na Ten Hag*

**MANCHESTER,** England

SCOTT McTominay amesema wachezaji wa Manchester United wako nyuma ya Kocha, Erik ten Hag, licha ya klabu hiyo kutokuwa na matokeo ya kuridhisha katika mechi za hivi karibuni.

McTominay alisema kuwa hali katika chumba cha kubadilishia nguo imekuwa "sawa" hakuna chochote kibaya kwa Ten Hag.

"Ni jukumu la wachezaji," alisema McTominay akinukuliwa na Sky Sport.

"Wachezaji wanajua hilo pia. Tumekuwa na wachezaji wengi wa ajabu na hivi sasa tuko kwenye hatua ambayo tuna wahusika wakubwa kwenye chumba cha kubadilishia nguo.

"Si tu kama baadhi ya makocha wengine ambapo imekuwa sumu kidogo wakati mwingine, wachezaji wapo nyuma ya kocha.

"Nimesema katika mahojiano mengine mengi na ndivyo itakavyokaa. Tumepata timu ya ajabu ya makocha pia inaweza kupotea kwa tafsiri ya kile wachezaji wanachofikiria na kinachosemwa nyuma ya milango, tunataka tu kufanya vema kwa klabu ya soka."

Kichapo cha Jumamosi dhidi ya Bournemouth kilikuwa cha 11 kwa United katika mechi 23 pekee msimu huu.



# Phillips aoneshwa mlango wa kutokea Man City

**MANCHESTER,** England

KALVIN Phillips yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na Manchester United majira ya joto, baada ya Manchester City kumwonesha mlango wa kutokea.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa England anaelekea kuondoka pale kwenye Dimba la Etihad huku Kocha Pep Guardiola wiki iliyopita akikiri kwamba haoni nafasi ya kumtumia kwenye kikosi chake.

Lakini, wadadisi wa mambo wanaeleza kuwa Kocha Mkuu wa Man United, Erik Ten Hag, ni shabiki mkubwa wa Phillips na anaona anafaa kwenye kikosi chake.

Chanzo hicho kilisema: "United wanaangalia hali ya Phillips kwa uangalifu sana. Ana uwezekano wa kwenda nje kwa mkopo Januari 2024, lakini atatafuta usajili wa kudumu.

"Yeye ni shabiki wa jinsi Phillips anavyocheza, na anadhani mtindo wake unafaa kabisa kwa United na kwa falsafa anayojaribu kuingiza kwenye timu.

"Pamoja na hayo, wawekezaji wapya wanataka klabu kuwekeza nguvu katika kujenga kikosi na kuendeleza wachezaji wa Uingereza, na Phillips bado anabakia kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Kiingereza katika Ligi Kuu.

"Haitakuwa mara ya kwanza kwa mchezaji kuhama kutoka City kwenda United, lakini huwa na utata."

Chanzo hicho kiliongeza: "Kuna hisia kwamba Guardiola angesimama katika njia ya Phillips. Uhamisho wa kwenda City haujafanikiwa na Guardiola anatamani hali hiyo kutatuliwa haraka iwezekanavyo."



## HABARI MICHEZO

# FGA Talents yatimua makocha baada ya vipigo Championship

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate Academy, maarufu FGA Talents, imemtimua Kocha Mkuu, Athumani Cairo na Msaidizi wake, Boniface Kiwale, baada ya mfululizo wa matokeo mabovu ya Ligi ya Champioship, inayoendelea.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, imeeleza mbali na kufikia makubaliano ya kuachana na makocha hao, imempata Ofisa Mtendaji Mkuu mpya, Mohamed Kambi, anayechukua nafasi ya Dk. Zemu Mbilu ambaye kuanzia sasa atakuwa ni Makamu Mwenyekiti.

"Tunapenda kuwataarifu kuwa tumefikia makubaliano ya kuachana na makocha wetu, Athumani Cairo na msaidizi wake Boniface Kiwale, kuanzia Desemba 11, 2023, timu sasa itakuwa chini ya kocha Catis Tully.

"Vilevile timu imefanya mabadiliko ya uongozi kwa kumteua Mohamed Aboud Kambi kuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa klabu akichukua nafasi ya Dk. Zemu Mbilu, ambaye sasa atakuwa Makamu Mwenyekiti wa Klabu na Rashid Hassan sasa atakuwa meneja wa timu," ilieleza taarifa ya klabu hiyo yenye maskani yake mjini Morogoro.

Mabadiliko hayo yanakuja siku chache tu baada ya kupokea kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa KenGold uliochezwa Uwanja wa Jamhuri, Morogoro, ilikuwa ni mfululizo wa matokeo mabaya ya timu hiyo msimu huu. Kabla ya hapo ilifungwa hapo hapo nyumbani mechi iliyopita dhidi ya Pamba FC.

# MAUTI ILIVYOMKUTA ZAHARA SAUZI, MUIMBAJI WA 'LOLIWE'

**Na Mwandishi Wetu**



MWIMBAJI wa kike aliyejipatia umaarufu mkubwa Afrika kwa wimbo wake uitwao 'Loliwe', Bulelwa Mkutukana maarufu kama Zahara, amefariki dunia nchini Afrika Kusini akiwa na umri wa miaka 36.

Waziri wa Sanaa, Michezo na Utamaduni nchini humo, Zizi Kodwa, alithibitisha kifo cha mwanamuziki huyo aliyekuwa akiimba na kupiga gitaa kilichotokea juzi, akisema ni masikitiko na pengo kubwa kwa muziki si nchini humo tu, bali Afrika nzima.

"Nimesitikishwa na kifo cha Zahara, natuma salamu za rambirambi kwa familia yake na tasnia yote ya muziki, serikali ilikuwa na familia katika kipindi hiki chote cha kulazwa kwake, yeye na gitaa lake wametengeneza kitu kikubwa sana ambacho kitabaki kuwa kumbukumbu katika muziki wa Afrika Kusini," alisema waziri huyo.

Awali, taarifa ya familia ilisema Zahara alikuwa amelazwa katika hospitali moja nchini humo bila kueleza zaidi, lakini taarifa za vyombo vya habari nchini Afrika Kusini zinaeleza alilazwa tangu Novemba 27 akiwa anasumbuliwa na ugonjwa wa ini.

**Kabla ya kifo chake, mwanamuziki huyo alikuwa akizushiwa kifo na mara kwa mara familia yake ililazimika kukanusha.**

Enzi za uhai wake. baada ya kipaji chake kuonekana alipata dili ya kurekodi kwenye Lebo ya TS Records na mwaka 2011 alitoa albamu iitwayo 'Loliwe' ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo iliyomtambulisha zaidi kwenye ulimwengu wa sanaa ya muziki kabla ya kurekodi albamu ya pili iitwayo 'Phendula' mwaka 2013, na akaendelea kufyatua singo na albamu mbalimbali zilizomfanya kutwaa tuzo mbalimbali barani Afrika.

**VINARA...**



Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Patrice Motsepe (katikati), akiwa na wanasoka bora Afrika 2023, Wanigeria Victor Osimhen (kushoto) na Asisat Oshoala, baada ya kukabidhiwa tuzo zao usiku wa kuamkia jana nchini Morocco.
**PICHA: MTANDAO**

# Benchikha ashusha mkata umeme

INATOKA UKURASA 24

mchezaji huyo kwa sababu atacheza moja kwa moja Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, kwani timu yake haikushiriki michuano yoyote inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho kwani msimu uliopita ilimaliza nafasi ya nane.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa awali Benchikha alitaka kuongeza wachezaji sita, lakini sasa ameongeza mpaka kufikia tisa wapya ambao wataongezwa kwa awamu, kipindi cha dirisha dogo linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 15, mwaka huu ambapo wataongezwa wachezaji kadhaa na msimu ujao kutafanyika usajili mwingine wa kumalizia idadi inayotakiwa.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alipotafutwa na gazeti hili kwa njia ya simu jana ili kuthibitisha mipango hiyo, alisema tayari kipindi cha usajili kinakuja hivyo tetesi hizo ni lazima zitakuwapo.

Alisema yeye anavyofahamu bado wanaendelea kucheza Ligi ya Mabingwa na sasa wanarejea kwenye Ligi Kuu, hivyo mpaka sasa hajui chochote kuhusu usajili na kama chochote kitatokea basi hatosita kuwaeleza wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

"Hiki ndicho kipindi chenyewe, tetesi zitakuwa nyingi sana mwisho wa siku wachezaji watakaosajiliwa watajulikana na kuonekana, sasa hivi sina chochote cha kuwaambia Wanasimba zaidi ya kukusanya nguvu zetu kwenda kuishangilia timu yetu, kwa sasa imeanza kutupa matumaini na nguvu mpya, kocha Benchikha naye ameleta mapinduzi mapya na amewaita mashabiki wajazane viwanjani, naomba turudi uwanjani kwa sababu mpira wetu ule tunaoupenda umerudi," alisema Ahmed.

Ijumaa ijayo Simba itacheza dhidi ya Kagera Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu, kabla ya kurudiana na Wydad Casablanca, Jumanne ijayo ukiwa ni mchezo wa raundi ya nne ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Yanga yatangaza vita...

INATOKA UKURASA 24

Alisisitiza kuwa licha ya Mtibwa Sugar kuwa katika hali mbaya kimatokeo, wanatakiwa kucheza kwa kuwaheshimu kwa sababu ni timu yenye watu wenye uzoefu mkubwa kwenye ligi na wanaweza kubadili kwao.

Baada ya Mtibwa Sugar, kikosi cha Yanga kitarudi tena dimba Desemba 20, kurudiana na Medeama FC, kisha watakutana ugenini dhidi ya Tabora United mchezo wa Ligi Kuu, hiyo ikiwa ni kama bandika bandua.

Wananchi hao watakuwa na mawindoni tena Desemba 26, dhidi ya Kagera Sugar halafu Tanzania Prisons na baadaye watarejea nyumbani kuvaana na Mashujaa FC, kwenye dimba la Azam.

Kwa upande wa Simba, wao watashuka dimbani Ijumaa wiki hii kuikaribisha Kagera Sugar, kisha Jumanne ijayo watakuwa wenyeji wa Wydad Casablanca ya Morocco katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kisha watakuwa wageni wa KMC Desemba 23.

Baada ya mchezo huo watasafiri hadi Kigoma kuivaa Mashujaa FC Desemba 26 na kisha siku mbili kabla ya mwaka kupinduka wataifuta Tabora United.

Michezo
Jumatano Desemba 13, 2023
Nipashe



Mauti ilivyomkuta Zahara Sauzi UKURASA 23



Erick Mbangossoum

# BENCHIKHA ASHUSHA MKATA UMEME WA MILIONI 590/- SIMBA

## Ni kitasa wa Chad anayevaana na Wydad, Raja Casablaca Ligi Kuu Morocco kwa miaka minne sasa...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ameanza kukisuka kikosi anachokihitaji, baada ya kuongea na kiungo mkabaji ('mkata umeme') raia wa Chad, Erick Mbangossoum, ajiunge naye kipindi cha dirisha dogo la usajili, imefahamika.

**Taarifa zinaeleza kuwa Benchikha alizungumza na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 na kimo cha mita 1.85, nchini Morocco wakati akiwa na kikosi cha Simba kilipokwenda kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ambapo pamoja na mambo mengine alikutana naye na baada ya hapo akaongea na uongozi wake kwani moja ya mapungufu yaliyopo kwenye kikosi ni kutokuwa na kiungo mkabaji asilia.**

Chanzo kinaeleza kuwa Benchikha alipata urahisi kwa kuteta na kiungo huyo kwani anacheza soka la kulipwa nchini Morocco katika Klabu ya Union Touarga Sport yenye maskani yake Rabat ikishiriki Ligi Kuu Morocco na kwa sasa ikishika nafasi ya 10 baada ya kujikusanyia pointi 14 katika michezo 10 kwenye ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

"Hana wasiwasi naye kwa sababu wanafahamiana, amemwambia aje Simba amfanyie kazi na tayari kocha ameshauambia uongozi na makubaliano yameshafanyika, thamani yake ni kulipa zaidi ya dola 235,000 sawa kiasi cha Sh. milioni 587 za Kitanzania hivi. Kwa sasa kuna mazungumzo tu ya kwanza yalipwe kwa awamu ngapi," kilisema chanzo hicho kikimzungumzia kiungo huyo aliyejiunga na Union Touarga Sport tangu Juni 2020.

Taarifa zinaeleza kuwa mpango utakapokamilika kwa asilimia 100, mchezaji huyo atafanyiwa vipimo vya afya nchini Tunisia na kusaini mkataba mrefu wa miaka mitatu.

"Baada ya hapo atasafiri kuja Tanzania na sisi tunakwenda kumsubiri Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere wasije kumuiba bure," alitania mtoa taarifa huyo.

Simba imekubali kumchukua

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yatangaza vita mpya ya pointi 18

**Na Saada Akida**

KLABU ya Yanga imesema Kocha wao Mkuu, Miguel Gamondi, atakuwa na kibarua kigumu zaidi mwezi huu, katika kuhakikisha timu hiyo inavuna pointi za kutosha kwenye jumla ya michezo sita ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na Ligi ya Mabingwa Afrika, kabla ya mwaka kupinduka.

Yanga katika mwezi huu watakuwa na michezo sita, mitano ya Ligi Kuu Bara wakianza kibarua hicho Jumamosi hii dhidi ya Mtibwa Sugar, kwenye dimba la Azam Complex na mmoja wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama ya Ghana Desemba 20, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Hata hivyo, wakati Yanga ikilia na ratiba ngumu, hali kama hiyo pia inaikumba Simba, ambayo nayo itakuwa na mechi sita kali za kuvuja jasho kupambania ushindi mwezi huu.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema mwezi huu maandalizi yake ni tofauti kwa sababu ukitazama ratiba ina michezo mingi na migumu.

Alisema kuna mechi iliyopo karibu dhidi ya Mtibwa Sugar, ambayo mbali na matatizo yao, lakini ni timu nzuri na hawataichukulia kama dhaifu kwa sababu wanaweza wakabadilika katika mchezo huo.


"Ukiangalia kalenda ya mwezi huu, ratiba imetubana sana kuna mechi nyingi ambazo ni ngumu sana, tunatakiwa kuvuna alama tatu dhidi ya Mtibwa Sugar, baadaye tunahitaji kushinda mbele ya Medeama katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tukimalizana na mechi hizo tunatakiwa kusafiri kwenda mikoani kwa ajili ya kucheza mechi zetu za ugenini, kuna Tabora United, Kagera Sugar na Tanzania Prisons na baadaye tunarudi nyumbani kukabiliana na Mashujaa FC," alisema Kamwe.

Aliongeza kuwa Kocha Gamondi anatakiwa kuandaa programu zake za kuwavusha Yanga salama katika mwezi huo kwa kufanikiwa katika malengo yao ya kusaka ushindi.

"Hatufanyi maandalizi ya mechi moja, bali mechi zote za Desemba. Msimamo wa ligi hautufurahishi kwa sasa, kazi kubwa ni kwa benchi la ufundi na wachezaji kutakiwa kupambana katika hiki kibarua kigumu kusaka alama tatu muhimu dhidi ya Mtibwa Sugar na kurejea katika nafasi yetu ya juu," alisema Kamwe.

INAENDELEA UKURASA 23



Miguel Gamondi

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >